**JELA** maisha kwa kumdhalilisha kijinsia mama miaka 55

UKURASA 5



**BALOZI** Marekani aisifu Tanzania uhuru wa habari

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Mei 3, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0580569

www.ippmedia.com


The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# RUZUKU CHADEMA

**MNYIKA** aanika yanayoendelea kati yao na Hazina, Msajili, wabunge 19... *Endelea Ukurasa 2*



John Mnyika



## Utouh: Rais awe mkali katika haya

UKURASA 2

## Samia kuhutubia Bunge la Kenya

UKURASA 2

**MICHEZO** USIYOYAJUA 'DABI' SIMBA NA YANGA JUMAMOSI HII UK. 14

MAONI, KATUNI UK. 6

# CHADEMA yafunguka kuhusu ruzuku

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema suala la ruzuku wanayostahili kupata haitatokani na wabunge wa viti maalum 19, waliokuwa wanachama wa chama hicho, ambao walishafukuzwa.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa CHADEMA taifa, John Mnyika, alisema viti maalum havichangii lolote kwenye ruzuku ya chama chochote cha siasa.

"Hadi sasa hatujapokea fedha yoyote kutoka Hazina wala Msajili wa Vyama vya Siasa kama inavyoelezwa... ni kama propaganda inafanyika kulazimisha kuwa viti maalum ndiyo vitaleta ruzuku kwenye chama," alisema Mnyika.

Alisema kumekuwa na upotoshaji mkubwa kuwa wabunge 19 ambao walishafukuzwa na chama hicho ndiyo watasaidia chama kipate ruzuku, na kwamba kikokotoo cha zuruku hakitumii wabunge wa viti maalum.

Alisema ruzuku hupatikana kwa idadi ya kura za ubunge kuanzia asilimia tano kuendelea na kiti cha ubunge wa jimbo katika uchaguzi mkuu.

"Ruzuku inayotajwa ya Sh. milioni 109 kama ndiyo, itatokana na kura za wabunge, viti maalum havihusiki kwa namna yoyote ile katika kupewa au kutokupewa ruzuku kwa chama chochote kile," alisema Mnyika.

Kwa mujibu wa Mnyika, kura za urais nazo hazina msaada wowote katika chama kupata ruzuku na ndiyo maana chama kinaweza kisiwe na mbunge hata mmoja, lakini kikapata ruzuku kutokana na kura za ubunge kuzidi asilimia tano.

Tangu wabunge 19 wa viti maalum kukubali kuapa na kuingia bungeni, kumekuwa na mvutano mkali, ikiwamo mijadala katika jamii.

CHADEMA inasema haijahusika kwa namna yoyote kutoa majina ya wabunge hao na wala hakuna aliyejaziwa fomu na kusainiwa na Katibu Mkuu wa chama kama sheria inavyoelekeza, lakini Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ilitangaza majina wa wabunge hao na waliapishwa Novemba 24, mwaka 2020 na Spika Job Ndugai.

Novemba 27, mwaka huu, CHADEMA ilitangaza kuwavua nyadhifa zao wabunge hao na kuwafuta uanachama.

Wabunge hao 19 walidai kuwa walikata rufani kwenye Baraza Kuu cha CHADEMA, ambalo hadi sasa halijakutana kupitia rufani hizo.

Katiba ya nchi imetaja aina za wabunge ni wa majimbo, viti maalum ambao lazima watokane na chama cha siasa na viti 10 vya rais. Wabunge hao 19 wa viti maalum ni Halima Mdee, Grace Tendega, Ester Matiko, Cecilia Pareso, Ester Bulaya na Agnesta Kaiza.

Wengine ni Nusrat Hanje, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Felister Njau na Naghenjwa Kaboyoka.

Pia, wamo Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Stela Fiayo, Anatropia Theonest, Salome Makamba, Conchesta Rwamlaza na Asia Mohammed.



Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhadj Mussa Salum (katikati) akijihudumia chakula wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na Benki ya CRDB katika hoteli ya Serena. Walioambatana naye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wapili kushoto) na Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omari Kumbilamoto. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Utouh: Rais awe mkali katika haya

**Na Sanula Athanas**

LEO ni siku ya 45 tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipoapishwa Machi 19, mwaka huu kushika madaraka hayo makubwa zaidi nchini kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli.

Kwa kipindi hicho cha mwezi mmoja na nusu, Rais Samia amefanya mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na kumpendekeza Dk. Philip Mpango kuwa Makamu wa Rais na kufanya mabadiliko katika baadhi ya nafasi za uongozi Ikulu, wizarani na taasisi za umma. Katika safari yake hiyo ya uongozi, aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ludovick Utouh, anamshauri Rais Samia kuwa mkali katika baadhi ya mambo.

Katika mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Utouh aliyekuwa CAG kwa kipindi cha miaka minane (2006-2014), pia alimshauri Rais Samia kuhakikisha miradi mikubwa iliyoanzishwa na serikali wakati wa uongozi wa Hayati Rais Magufuli inatekelezwa.

Alisema ni muhimu miradi hiyo kusimamiwa vizuri na kukamilishwa kwa kuwa tayari imeshaigharimu nchi kiwango kikubwa cha fedha.

Miradi mikubwa inayotekelezwa na serikali ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa bwawa la kufua umeme wa maji kwenye Mto Rufiji, ujenzi wa daraja refu zaidi Afrika Mashariki na Kati -- Daraja la Kigongo-Usisi na ununuzi wa ndege za serikali kwa lengo la kuliimarisha Shirika la Ndege (ATCL).

Ili miradi hiyo ikamilishwe, Utouh alisema kuna haja mwanafunzi wake huyo katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Rais Samia, awe mkali dhidi ya watendaji wazembe na wanaoendekeza rushwa na ufisadi.

"Ushauri wangu kwa Rais Samia, kwanza ajitahidi kwa kila hali hii miradi mikubwa ya kitaifa iliyoanzishwa ikamilike na ifanye kazi.

"Lakini kwa ajili ya kufanikisha hilo, ule umuhimu wa kisisitiza heshima ya watendaji kazi wa serikali unatakiwa kufuatwa.

"Uadilifu ni muhimu, watu wahesimu kazi, wapende kazi na wafanye kazi. Kaulimbiu ya 'Tanzania ya Kazi Iendelee', tuishi hiyo kaulimbiu hasa kwenye uadilifu.

"Ufisadi ukipamba moto kwenye nchi hii, hataweza kukusanya mapato ya kufanya haya anayotaka kuyafanya.

"Awe mkali na pale mtu anapokosa, asimwonee mtu aibu, akipata uthibitisho achukue hatua," alishauri.

Utouh ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, pia alimshauri Rais Samia kuhakikisha serikali yake inashirikiana vizuri na Sekta Binafsi.

Alionya kuwa nchi mbalimbali ambazo serikali zake zilijaribu kufanya biashara, hazikupata matokeo chanya.

"Serikali yake (Rais Samia) iweke wazi kwamba hii nchi ikiwa hakuna Sekta Binafsi zilizo imara, hatutafika.

"Nchi nyingi zilijaribu kufanya biashara. Hata Tanzania tuliwahi kujaribu kufanya biashara, lakini tulifika mahali tukabinafsisha.

"Kwa hiyo, kwa kuwa ni kitu ambacho kilishajaribishwa na hakijaleta matokeo, kuwe na uaminifu, watu watii sheria bila shuruti na kwa pamoja tuone kwamba tuna wajibu wa kusukuma maendeleo ya nchi yetu mbele," alishauri.

Katika mahojiano hayo na Nipashe, Utouh alizungumzia mambo mengine mbalimbali ya kitaifa yakiwamo yanayohusu uwekezaji na biashara, uwajibikaji na yanayoigusa Sekta ya Elimu.

***USIKOSE KUFUATILIA KESHO, UTOUH AKISHAURI JAMBO NYETI KWENYE SEKTA YA ELIMU**

# Samia kuhutubia Bunge la Kenya

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufanya ziara rasmi ya siku mbili katika Jamhuri ya Kenya kuanzia kesho kwa mwaliko wa Rais Uhuru Kenyatta.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, ilibainisha kuwa akiwa Kenya, Rais Samia atakuwa na mazungumzo rasmi na mwenyeji wake, Rais Kenyatta, kisha atalihutubia Bunge la Kenya litakalojumuisha wabunge wa mabunge yote mawili ya nchi hiyo.


"Rais Samia atahudhuria na kuhutubia mkutano wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Kenya na Tanzania utakaofanyika jijini Nairobi kwa lengo la kujadiliana masuala mbalimbali yahusuyo fursa za biashara na uwekezaji zilizopo Tanzania na Kenya," Msigwa alisema katika taarifa yake hiyo.

Alisema matukio ya ziara hiyo yatarushwa mubashara na vyombo vya habari vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Hiyo ni ziara ya pili kwa Rais Samia nje ya nchi tangu aapishwe kushika madaraka hayo Machi 19, mwaka huu kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli.

Mwezi uliopita, Samia alizuru Uganda ambako pamoja na mambo mengine, Tanzania ilitiliana saini na nchi hiyo kutekeleza mikataba mitatu yenye nia ya kuendeleza sekta ya mafuta na gesi.

TANGAZO


DR. REGINALD MENGI
HAKIKA AMEACHA ALAMA
1942 – 2019
IPP
Will Always Care For You

# Balozi Marekani ampongeza Rais Samia uhuru wa habari

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Marekani nchini, Donald Wright, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa, jambo linalotoa tumaini jipya katika ukuaji wa sekta hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ubalozi huo nchini ambayo ni maoni yake binafsi kuhusu maadhisho ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari yanayofanyika leo jijini Arusha, uamuzi wa Rais Samia kushughulikia vikwazo kandamizi kwa vyombo vya habari ikiwamo kushughulikia masuala ya kisheria yanayokwaza utendaji wa waandishi wa habari ni hatua kubwa.

"Ninafahamu kuwa hivi karibuni serikali itaunda kamati ya kupitia sheria zilizopo ikiwa ni pamoja na zile zinazokwaza uhuru wa habari na vyombo vya habari. Ninapongeza hatua hizi muhimu na kuwahimiza wadau wote wa habari kuzipokea kwa nia njema na dhamira safi pamoja na kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria zilizokwaza uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania katika miaka ya hivi karibuni," alisema.

Kwa mujibu wa Balozi huyo, ametiwa moyo na hatua zilizochukuliwa hivi karibuni na serikali kuwawajibisha wanaowatisha na kuwanyanyasa waandishi wa habari.

"Ni matumaini yangu kuwa hatua hizi zitapanuliwa zaidi katika siku zijazo, hivyo kwa mara nyingine tena, waandishi wa habari wa Tanzania watapata uhuru na nafasi ya kufanya kazi yao," alisema.



Balozi Wright alisema siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani inatoa fursa ya kuenzi nafasi na wajibu muhimu wa vyombo huru vya habari katika kuimarisha na kuhifadhi jamii zilizo huru na kuangazia kazi adhimu inayofanywa na waandishi wa habari, vyombo vya habari, wahariri, wafanyakazi na wengine katika vyumba vya habari, studio na vituo vya redio za kijamii duniani kote kuwaelimisha na kuwahabarisha raia kuhusu masuala mbalimbali ya siku hadi siku.

Alisema siku hiyo ni fursa ya kubainisha na kukumbusha kuhusu vitisho vikubwa vinavyowakabili waandishi na taasisi hizo za habari wakati zikitekeleza kazi yao hiyo muhimu, na kwamba muhimu zaidi kuliko wakati mwingine wowote, kuazimia na kujitoa kwa dhati kusaidia uhuru wa vyombo vya habari.

"Toka nilipowasili Tanzania mwaka jana, nimejiwekea utaratibu wa kuwatafuta waandishi wa habari na kusikiliza simulizi zao. Ninafahamu kuwa wanakabiliwa na changamoto kubwa sana, kutoka mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia yanayotikisa misingi ya uandishi wa habari, kuzuka kwa mitandao na kueneza taarifa za uongo na uzushi," alisema na kuongeza:

"Haijawahi kutokea kuwa vigumu zaidi kuwa mwandishi wa habari Tanzania kama ilivyo sasa. Isitoshe, janga la Covid-19 limeongeza maradufu kila moja ya changamoto hizi."

"Lakini pamoja na vikwazo vyote hivi, nina matumaini kuwa bado kuna mustakabali mwema kwa uhuru wa tasnia ya habari nchini Tanzania."

Balozi huyo alisema kuhusu hitaji la kwenda na mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia, anatiwa moyo na vyombo kadhaa vipya vya habari vilivyokubali kupokea teknolojia mpya katika uendeshaji na ufanyaji wake biashara.

"Serikali ya Marekani inafadhili programu kadhaa za kusaidia maendeleo ya vyombo vya habari, zinazofanya kazi na wamiliki wa vyombo vya habari katika kubuni na kuboresha mbinu mpya za kibiashara zenye ufanisi zaidi. Nina matumaini makubwa kwamba jitihada hizi zitazaa matunda," alibainisha.

**"Ninafahamu kuwa hivi karibuni serikali itaunda kamati ya kupitia sheria zilizopo ikiwa ni pamoja na zile zinazokwaza uhuru wa habari na vyombo vya habari. Ninapongeza hatua hizi muhimu na kuwahimiza wadau wote wa habari kuzipokea kwa nia njema na dhamira safi pamoja na kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria zilizokwaza uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania katika miaka ya hivi karibuni," alisema.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU TANZANIA**
**ARUSHA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 9 LA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YA**
**JACOB ALFRED OMBAY……………MAREHEMU**
**NA**
**ALFRED JACOB OMBAY**
**NICODEMUS JACOB OMBAY**
**VICTORIA JACOB OMBAY**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 mwezi wa sita mwaka wa 2021.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe
22 mwezi wa nne mwaka 2021.

R. B. Massam
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
ARUSHA.

# Wafanyabiashara wataka ufafanuzi ahueni bidhaa kutoka Z'bar

**Na Waandishi Wetu**

SIKU chache baada ya serikali kutangaza kupunguza gharama za kushusha mizigo inayotoka Zanzibar katika Bandari ya Dar es Salaam, Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (CWT), imetaka ufafanuzi zaidi wa viwango na bidhaa zenyewe.

Wiki iliyopita, Nipashe ilichapisha habari kuhusu kushushwa kwa gharama hizo ikiwa ni hatua ya kuzipatia ufumbuzi na kuziondoa kero tano za Muungano ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kwa muda na wananchi wa pande zinazohusika na Muungano.

Katibu Mkuu wa JWT, Abdallah Mwinyi, akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, alisema ukiondoa matatizo ya mizigo midogo kilo tano au 10 za bidhaa, zipo kero kubwa za kibiashara kwenye bidhaa kutoka Zanzibar.

"Huwezi ukatoa bidhaa ukashushia Zanzibar halafu kwa kodi ya Zanzibar utakayolipa mzigo uingize Bara kwa gharama zilezile ulizofanya kule, hii maana yake Bandari ya Dar es Salaam haitafanya kazi kama itakuwa hivyo," alisema.

Mwinyi alisema ili suala hilo lifanyike na bandari zote zifanye kazi vizuri, lazima waangalie Bandari ya Dar es Salaam ambayo ndiyo kubwa kwa kuangalia viwango vya kodi vifanane na Zanzibar.

"Lazima waangalie uwiano wa kodi wa pande zote mbili ili usiathiri bandari nyingine, lakini kwa kusema watapunguza bila kutaja viwango na bidhaa zenyewe kuna ukakasi, watufafanulie ni bidhaa zipi?" alihoji.

Wakati jumuiya hiyo ikiyasema hayo, baadhi ya wananchi wa Zanzibar wamepongeza hatua hiyo na kubainisha kuwa itapunguza ukali wa maisha.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema gharama wanazotozwa kutoa bidhaa Zanzibar kwenda Tanzania Bara zinawaumiza hasa ikizingatiwa kuwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanatozwa kodi mara mbili -- za Mamlaka ya Mapato (TRA) na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB).

Juma Ali Khatib, Mwenyekiti wa Chama cha ADA Tadea, alisema hatua hiyo ni nzuri na imekuja kwa muda mwafaka kwa sababu Tanzania ni nchi moja, hivyo siyo vyema mtu anapotoka Zanzibar na bidhaa kwenda Bara kulipishwa ushuru mara mbili.

"Huu ndiyo Muungano tunaoutaka, yaliyokuwa yakifanyika, yalikuwa yanaumiza upande mmoja wa Muungano. Sisi kama Chama cha ADA Tadea tunapongeza hatua hiyo," alisifu.

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Umma wa Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Salum Bimani, alisema hatua hiyo ni nzuri, lakini kuna kero zingine kubwa za Muungano zinazotakiwa kufanyiwa kazi ikiwamo ya Mfuko wa Pamoja wa Muungano.

Alidai kuwa mfuko huo ambao ulianzishwa mwaka 1984 haujaunufaisha upande mmoja wa Muungano.

"Huu ni Muungano wa nchi mbili na ulikuwa na makubaliano na siyo mmoja awe mkubwa na mwingine mdogo, nchi mbili zote ziwe huru," alisema Bimani.

Rashid Mchenga, mkazi wa Mjini Unguja, alisema Tanzania ni nchi moja, hivyo ni vyema kuwa na kodi moja ili kuwapunguzia ukali wa maisha wafanyabiashara wa Zanzibar.

Alisema hatua hiyo ya kuondoa tozo hiyo ni nzuri lakini usimamizi wake uwe mzuri kwa kuwa kama hawatakuwa makini, serikali itakosa mapato, akitahadharisha kuwa wafanyabiashara wote kutoka Tanzania Bara wataelemea Zanzibar kushusha biashara zao.

Mariyam Juma, mkazi wa Amani Zanzibar, alisema wanapotoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam, wanashindwa hata kuwachukulia zawadi ndugu na jamaa zao kwa hofu kutozwa kodi bandarini.



# Maisha jela kumdhalilisha kijinsia mama wa miaka 55

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Naunambe, Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, Ally Chikukuru (21), amehukumiwa kutumikia kifungo cha maisha gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kumlawiti kwa nguvu mama mwenye umri wa miaka 55. Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Ruangwa, Raula Shehagilo, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kuomba aonewe huruma akidai haikuwa nia yake bali ilichangiwa na ibilisi wa mapenzi na kujikuta akifanya tendo hilo bila ya kukusudia.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Shehagilo alimuuliza Mwendesha Mashtaka Mkaguzi wa Polisi, Bocho Monata, iwapo ana kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hakuwa nazo, lakini aliiomba mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

Akitoa hukumu, hakimu alisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili, lakini kufuatia ukubwa wa kosa, kifungu cha sheria 154 (a) (2) (2), sura ya 16/2019 anamhukumu kutumikia kifungo cha maisha jela.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka Monata, kuwa Novemba 15, mwaka jana, huko Kijiji cha Naunambe, Wilaya ya Ruangwa na Mkoa wa Lindi, mshtakiwa alikwenda nyumbani kwa mlalamikaji na kumlawiti kwa nguvu.



Mratibu wa Mafunzo kutoka LHRC, Joram Bwile, akiendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kujiamini na kujitambua katika kuisaidia jamii kutatua tatizo la ukatili wa kijinsia kwenye maeneo yao wasichana wadogo na waliojifungua chini ya miaka 18 kutoka kata nane za Halmashauri ya Manispaa ya Kahama jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TBS yakagua magari 600 kutoka ughaibuni

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limekagua magari 626 kutoka nje ya nchi na kati yake, 211 yamekutwa na kasoro mbalimbali.

Ofisa wa Masoko wa TBS, Deborah Haule, aliliambia Nipashe mwishoni mwa wiki kuwa, kati ya magari hayo yaliyokutwa na kasoro, asilimia 85 zimetokana na uchakavu wa magurudumu.

"Tumeshakagua magari 626. Kati ya hayo, magari 211 yamekutwa na kasoro ndogondogo na magari 415 hayakuwa na kasoro," alibainisha.

Kaule alisema kati ya magari hayo yenye kasoro, 51 yamerekebishwa na kufaulu katika ukaguzi wa pili.

Alisema magari mengine yaliyobaki bado yapo kwenye hatua mbalimbali za matengenezo.

Kuhusu gharama za matengenezo ambazo baadhi ya watu wanazilalamikia kuwa juu, Haule alisema TBS haihusiki na kwamba gharama zinajulikana kwa mwenye gari.

"Gharama zinajulikana kwa mwenye gari. Hii ni kutokana na TBS kutokujihusisha na utengenezaji wa kasoro zilizobainika wakati wa ukaguzi," alisema.

Kaule alisema kati ya kasoro zinazojitokeza, asilimia 85 ya kasoro hizo ni uchakavu wa magurudumu na mwenye gari hushauriwa kubadili kwa ajili ya usalama wake.

Alisema mpaka sasa vituo vya ukaguzi vina jumla ya wataalamu 31 ambao ni wa uhandisi mitambo na magari.

Alisema wataalamu hao wamepatiwa mafunzo ya ziada katika viwango vya magari na matumizi ya vifaa vya ukaguzi.

TBS sasa inatekeleza jukumu hilo baada ya serikali kuagiza ukaguzi wa magari yanayoagizwa kutoka nje ya nchi ufanywe na taasisi badala ya ukaguzi kufanyika kwenye nchi yanakotolewa.

## MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TASAF

TASAF
TANZANIA SOCIAL ACTION FUND
MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

## UTAMBUZI NA UANDIKISHAJI WA WALENGWA

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umeanza zoezi la utambuzi na uandikishaji wa kaya za walengwa wanaokidhi vigezo vya kusaidiwa na Mfuko kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Zoezi hilo litakamilisha utambuzi wa asilimia 30 ya kaya ambazo hazikufikiwa katika kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Tatu kilichotekelezwa kuanzia 2013 hadi 2019.

Zoezi la utambuzi na uandikishaji wa walengwa linafanyika kwa awamu na litaendelea hadi mwezi Julai 2021. Mzunguko wa Kwanza umekamilika katika Halmashauri zote za mikoa ya Pwani, Ruvuma, Dodoma, Lindi, Mtwara na Wilaya zote za Unguja na Pemba. Kaya zinazotambuliwa zinahojiwa kupata taarifa zake kwa kujaziwa dodoso. Hatua ya pili ni kuchakata taarifa zilizokusanywa ili kupata kaya zilizokidhi vigezo ambazo zitaandikishwa kwenye daftari la kaya za walengwa.

Mzunguko wa Pili wa utambuzi na uandikishaji wa kaya za walengwa utafanyika mwezi Mei 2021 katika halmashauri zote za mikoa ya Singida, Geita, Mwanza, Simiyu, Kigoma, Katavi na Rukwa. Viongozi wa Vijiji na Mitaa katika maeneo hayo mnatakiwa kuwatangazia na kuwahamasisha wananchi wote katika maeneo husika kuhudhuria mikutano ya utambuzi wa walengwa kwa ratiba itakayopangwa. Zoezi la utambuzi na uandikishaji litafanywa na Timu za wawezeshaji kutoka halmashauri husika na litasimamiwa na Viongozi wa Vijiji na Mitaa. Wajibu wa Viongozi ni kuhakikisha kwamba zoezi la utambuzi linafanywa kwa haki na weledi bila upendeleo au ukiukwaji wa taratibu ili kupata **walengwa wanaokidhi vigezo vilivyowekwa.** Viongozi wa Vijiji/Mitaa/Shehia watakaobainika kuharibu zoezi la utambuzi na kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi, watawajibika katika ngazi zao za usimamizi kwa mujibu wa viapo walivyokula na kutia saini.

Aidha, Wananchi wote mnahimizwa kuhudhuria mikutano hiyo pale itakapoitishwa katika maeneo yenu na kuzingatia maelezo na taratibu zilizowekwa ili kupata orodha sahihi ya watu wanaokidhi vigezo vya kuandikishwa kwenye Mpango wa TASAF.

Idadi ya walengwa kwa Kipindi hiki cha Pili cha Awamu ya Tatu (2020 – 2023) ni Kaya 1,400,000. Walengwa watakaoandikishwa watawezeshwa kujikwamua kiuchumi kwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundo mbinu ya elimu, afya na maji kupitia ajira za muda na kuanzisha miradi ya ujasiriamali hivyo kujiongezea kipato.

Ladislaus J. Mwamanga
**MKURUGENZI MTENDAJI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba jipangeni CAF, Kaizer Chiefs si wepesi

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, tayari wamefahamu wapinzani wao katika hatua ya robo fainali inayotarajiwa kupigwa kati ya Mei 14-15, kabla ya kurudiana Mei 21-22, mwaka huu, ambapo itaanzia ugenini dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Tangu kupangwa kwa droo hiyo mashabiki, wanachama na hata baadhi ya viongozi wa Simba wameipokea kwa mikono miwili huku wakiweka wazi kuwa safari ya kutinga nusu fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), ni nyepesi kwao.

Simba ambayo kama ikivuka hatua hiyo itakutana na mshindi kati ya Wydad Casablanca ya Morocco ama MC Alger ya Algeria, wanaona droo hiyo imekuwa nyepesi na ingekuwa ngumu zaidi kwao endapo wangeangukia kwa timu kutoka Afrika Kaskazini (Uarabuni) MC Alger ama CR Belouizdad za Algeria.

Uongozi wa Simba, mbali ya kuwaona Kaizer Chiefs ni wepesi kwao kutokana na tamaduni za Afrika Kusini kutotofautiana sana na Afrika Mashariki hususan upande wa 'siasa' za soka, lakini kutawapunguzia usumbufu wa kusafiri umbali mrefu.

Hata hivyo, kwenye hatua ya makundi, Kaizer Chiefs imepenya kutokana na kanuni ya 'Head to Head' (matokeo zilipokutana) dhidi ya Horoya FC ya Guinea kutokana na timu hizo kila moja kumaliza na pointi tisa nyuma ya vinara wa Kundi lao la C, Wydad Casablanca waliohitimisha kileleni na pointi zake 13, huku Petro de Luanda ikiburuza mkia na alama yake moja.

Katika mechi zake sita za hatua za makundi, Kaizer Chiefs imeshinda mbili, sare tatu na kupoteza mchezo mmoja, huku ikifunga mabao matano tu na kuruhusu nyavu zake kutikiswa mara sita.

Lakini kama ni kitakwimu, Simba ipo juu zaidi kwani imeongoza Kundi lake la A ikiwa na alama 13, lililokuwa likiundwa na bingwa mtetezi wa michuano hiyo, Al Ahly ya Misri iliyomaliza nafasi ya pili na pointi 11, AS Vita ya DR Congo iliyoshika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba Al-Merrikh ya Sudan iliyoburuza mkia na alama zake mbili.

Hata kwa upande wa takwimu za mabao, Simba ipo juu zaidi ya Kaizer Chiefs kwani yenyewe imeruhusu nyavu zake kutikiswa mara mbili pekee huku ikizifumania nyavu za wapinzani mara tisa.

Pamoja na takwimu hizo za kuvutia za Simba, hiyo haitoshi kubweteka na kujiaminisha kwamba imepata mpinzani mwepesi katika hatua hiyo, kwani mara nyingine mpira wa miguu una matokeo ya kushangaza hasa unapokwenda na matokeo yako uwanjani na kujiamini kupita kiasi.

Nipashe tunakiri kwa sasa Simba ipo kwenye kiwango cha juu na ni moja ya timu zinazoogopwa katika michuano hiyo, lakini hilo haliwezi kuwa sababu kwao ya kuamini kwamba Kaizer Chiefs watakuwa wepesi na kuacha kujiandaa ipasavyo.

Tunaamini njia pekee ya Simba kufanya vizuri, kwanza ni kufanya maandalizi ya kutosha na kumheshimu mpinzani wake kuelekea mechi hiyo ya robo fainali ambayo ni mtoano.

Ikumbukwe katika hatua ya makundi, pamoja na ubora wa kiwango cha juu wa Wydad Casablanca, ilikubali kipigo cha mabao 4-0 nyumbani dhidi ya Kaizer Chiefs na Jumapili ya Aprili 25, mwaka huu ikawatembezea kichapo cha mabao 2-1 nyumbani kwa majirani zao wa Afrika Kusini, Memelodi Sundowns kwenye mechi ya Ligi Kuu ya nchini humo.

Sote tunafahamu ubora wa Mamelodi katika michuano hiyo ya CAF ambayo nayo imemaliza kileleni mwa msimamo wa Kundi B ikiwa na pointi 13, hivyo kamwe Simba hawapaswi kuichukulia poa Kaizer Chiefs kwani inaweza kujikuta inatoka vichwa chini na wapinzani wao hao kusonga mbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la Asukile na tuhuma za rushwa Yanga limulikwe zaidi

Na Adam Fungamwango

**AKIWA** na hasira ya kufungwa, nahodha wa timu ya Prisons, Benjamin Asukile, baada ya mechi dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, aliongea maneno ambayo yamekuwa gumzo kubwa kwa mashabiki wa soka nchini.

Alisema mengi, akianzia kunyimwa penalti na walipokwenda kumuuliza mwamuzi akadai kuwa haoni. Mtangazaji aliyemhoji alimkatisha kidogo, lakini Asukile alionekana kutopendezwa na kitendo hicho. Mwishoni akasema anashangaa kwa baadhi ya timu kutumia gharama kubwa kusajili wachezaji kutoka nje, lakini wachezaji hao wanashindwa kucheza mpira, badala yake wanalazimisha kushinda kwa kutumia hila.

Ukiisikiliza na kuangalia mahojiano yale, ni kwamba mtangazaji hakutaka mchezaji kutoa tuhuma zile kwa sababu hazikuwa na ushahidi. Lakini pia ukiangalia ni kwamba, mtangazaji alitaka mchezaji huyo kuendelea kumtuhumu mwamuzi na ilionekana hakuwa na shida na hilo.

Tatizo lake lilikuwa ni tuhuma za rushwa tu dhidi ya timu pinzani na Prisons. Kwa maoni yangu, wote walikuwa sahihi. Mtangazaji alichoamini ni hicho. Hakutaka kituo chake kiwe ndiyo chanzo cha tuhuma zile nzito za rushwa.

Asukile naye alikuwa sahihi. Aliwasilisha kile ambacho anakijua na anakiamini. Tatizo lake labda alikuwa na hasira aliyotoka nayo uwanjani. Sina tatizo na mtangazaji wala mchezaji. Kila mtu ametekeleza kile ambacho anaamini.

Nilichoshangaa ni kuona baadhi ya wachambuzi wakimuona Asukile kwamba hakuwa na uhakika, wala ushahidi na kile alichokisema zaidi ya jazba tu ya kufungwa. Inawezekani ni kweli, lakini utafiti au uchunguzi umefanyika?

Nilitegemea sasa waandishi wa habari kusaka ukweli wa hilo. Waandishi wa Habari za Uchunguzi wanaweza kuingia mzigoni na kutuletea habari iliyo sahihi. anaweza kutueleza wazi kuwa matokeo ya uchunguzi wao ni kweli au Asukile hakuwa mkweli.

Navyoona ni kwamba waandishi wa michezo wanadhani kwamba jambo hili haliwahusu na linahusu mamlaka husika pekee kama Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) pekee.

Asukile kwa sasa ametulia, hana jazba tena na inawezekana kabisa kwenda kumuuliza taratibu, atasema kwamba ilikuwa ni hasira tua au ni kweli. Anaweza kutoa namba za watu ambao wamepiga. Zinaweza kuwa siyo namba za watu husika, labda zimetumiwa tu. Je wanaomiliki namba hizo wana nasaba na watu wanaotuhumiwa? Na mengi yanayofanana na hayo. Kwenye habari kama hizi ni lazima mwandishi awe kama mpelelezi halisi. Ukiangalia kila kitu au kila unachokitafuta kwa jicho la tatu.

Wakati mwingine hata serikali hutumia uchunguzi uliofanywa na waandishi kutatua tatizo, au kulishughulikia. Si kwenye siasa, au kijamii tu, bali hata kwenye michezo.

Mwandishi Sanula Athanas wa Nipashe, aliwahi kupata tuzo tatu za Mwandishi Bora wa Michezo kwa habari tatu za uchunguzi za michezo kwa nyakati tofauti. Moja ni ya upangaji wa matokeo kwenye Ligi Kuu.

Nyingine ni ubebwaji wa pesa za milangoni kwenye viroba na pia habari ya uchunguzi ya pesa za wachezaji na makocha kwenye soka kutokatwa kodi. Serikali ilifanyia kazi hili kwa kuleta tiketi za kieletroniki na pia sasa wachezaji na makocha wote wanakatwa kodi.

Hata hili, waandishi wachunguze na kuja na majibu, vyombo vya serikali navyo vinaweza kuingia walipoishia na wao kujidhihirisha, kama walivyofanya huko nyuma.

Kama tunataka kusaidia mpira wetu kwa sasa, ni wakati wa kutofumbia macho kero kama hizi zinazoibuliwa na wachezaji na mashabiki.

HABARI KITAIFA

# CRDB yawafuturisha wateja wake

**Na Elizabeth Zaya**

KATIKA kusheherekea mwezi Mtukufu wa Ramadhan, Benki ya ya CRDB imeandaa futari kwa wateja wake katika mkoa wa Dar es Salaam zaidi ya 400.

Miongoni mwa waliohudhuria katika hafla hiyo ni Shehe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhadj Mussa Salum.

Akizungumzia katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema benki hiyo inawachukulia wateja wake kama sehemu ya familia yake, na kwamba katika mwezi huu mtakatifu inatoa fursa ya kushirikiana kuboresha mahusiano kwa ushiriki pamoja kupitia ibada ya funga na futari.

"Tunatumia kipindi hiki pia kuonyesha shukrani zetu kwao kwa kuendelea kuichagua benki yetu, na wakati huo huo tunathibitisha kujitolea kwetu kwa kuelewa mahitaji yao na matarajio yao," alisisema Nsekela.

Nsekelea alisema mbali na kufuturisha wateja, benki hiyo pia imekuwa ikitoa msaada wa futari kwa vituo vya kulelea watoto vyenye uhitaji mkubwa, na kwamba kwa mwaka huu imetenga Sh. milioni 100 kwa ajili ya kusaidia futari kwa vituo 40 vya kulelea watoto katika kanda zote nchini.

Akitoa shukrani kwaniaba ya wageni waalikwa, Shehe Salum alishukuru na kuipongeza benki hiyo kwa kuuandaa futari hiyo pamoja na kutoa misaada kwa watoto wanaolelewa katika vituo vya watoto yatima katika mwezi huu.

Alisema katika kipindi hiki ni vema walio na uwezo kiuchumi kuwafuturisha wasio na uwezo ili kujiongezea thawabu, kusoma maneno ya Mungu kwa wingi, kusali na kufanya mema, huku wakijitenga na mabaya.

# NHIF yaonya maduka yanayokiuka mikataba

**Na Richard Makore,** GEITA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), mkoani Geita, umewaonya wamiliki wa maduka ya dawa za binadamu wanaokiuka mikataba na kubagua wanachama wa mfuko huo wanaofika kwao kupata huduma.

Onyo hilo lilitolewa hivi karibuni na meneja wa mfuko huo mkoani Geita, Elius Othiombo, alipozungumza na waandishi wa habari, kuhusu baadhi wa wamiliki wa maduka hayo kutoa huduma kwa ubaguzi. Hivi karibuni mkoani humo, baadhi ya wananchi walilalamikia maduka hayo kuwa yanabagua wananchama wa mfuko huo. Walisema wamiliki hao wanawabagua na wengine kuwaambia kwamba wakitaka huduma hiyo wanatakiwa kuandikiwa cheti cha kununua dawa kutoka hospitali wanazotaka wao.

Othiombo alisema Mkoa wa Geita una jumla ya maduka 12 waliyoingia nayo mkataba wa kuhudumia wanachama pamoja na vituo vya kutolea huduma 174.

Aidha, alisema Geita Mjini kuna hospitali nne walizoingia nazo mkataba na maduka manne ya kuuza dawa za binadamu.

"Kama kuna duka linaweka masharti, mgonjwa fulani ili apate huduma ni lazima aandikiwe cheti cha kununua dawa kutoka hospitali wanayotaka wao, tutasitisha mkataba na wao, tunataka kila mwanachama wetu apate huduma bila masharti," alisema.

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF MOSHI)**
**PETITION NO 04 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE COMPANIES ACT, CAP 212**
**AND**
**ADVERTISEMENT OF WINDING UP PETITION**
**(PURSUANT TO SECTION 281 OF THE COMPANIES ACT, CAP 212)**

**IN THE MATTER OF** — **MSOKE NASHALO FARMS LIMITED**

A Petition to wind up the above named company of

**Address** — **MSOKE NASHALO FARMS LIMITED**
**HOUSE NO. 44 CHAGGA STREET**
**P. O. BOX 569, MOSHI, TANZANIA**

**Presented on** — 30th day of March, 2021

**BY:**
**Names of address of Petitioner** — DAPHROSA EDITH MUSHI OF P. O. BOX 10221 DAR ES SALAAM

Claiming to be contributory of the company

**Will be heard at:** — IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA IN THE HIGH COURT OF TANZANIA MOSHI DISTRICT REGISTRY AT MOSHI

**On (date)** — 10TH MAY, 2021

**At (Time)** — 09.00 AM O' CLOCK IN THE FORENOON

(Or as soon thereafter as the Petition can be heard)

Any person intending to appear on the hearing of the Petition (whether to support it or to oppose it) must give notice of his intention to do so to the Petitioners or his / Advocate in accordance with Rule 104 of the Companies (Insolvency Rules) 2004 by 16:00 hours on the business day before the dated of the hearing given above.

The Petitioner's Advocates is — Imara Law Consult Advocates, 3rd Floor, Avalon Building, P. O. Box 7575, **Dar es Salaam.**

**DATED : 14TH March, 2021**

# HakiElimu yaja na mwarobaini wa upungufu sera ya elimu

**Na Elizabeth Zaya**

RIPOTI ya HakiElimu imeainisha baadhi ya upungufu katika Sera ya Elimu ya mwaka 2014 nchini, huku ikitoa mapendekezo katika baadhi ya maeneo yanayohitaji kuboreshwa zaidi.

Akichambua matokeo ya ripoti hiyo, Mshauri Mwelekezi wa HakiElimu, Dk. Wilberforce Meena, alisema miongoni mwa maeneo ambayo ripoti hiyo inapendekeza kufanyiwa maboresho ni pamoja na kutofautiana kwa falsafa ya kitaifa na sera hiyo, kutokuhusisha ushahidi wa kutosheleza wa kitafiti kwa kila sekta ndogo ya elimu.

Nyingine ni kushindwa kutoa mwongozo kwa kila changamoto isipokuwa ahadi nyingi ambazo ni ngumu kutekelezeka, kutokuzingatia uendelevu na kutofautiana na sera nyingine zilizotangulia ikiwamo ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995 na kushindwa kugawa majukumu kwa wadau mahususi wa elimu ili kukuza uwajibikaji kwenye tekelezaji.

Pia, HakiElimu ilipendekeza kuwapo na mpangilio, muundo, maudhui na utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo katika masuala ya kisera.

"Sera haijatamka lengo kuu na malengo ya elimu ya kitaifa kwa kila sekta ndogo ya elimu, imetoa tamko la ujumla katika kushughulikia sekta ya elimu badala ya kutoa matamko mahususi yanayolenga sekta ndogo ndogo za elimu, imekosa mkakati wa utekelezaji na msukumo wa kisheria," alisema Dk. Meena.

"Uandaaji wa sera haukuwashirikisha kikamilifu wadau wa elimu, hivyo kuchangia kuwapo kwa mapungufu mengi, lugha iliyotumika kwenye sera haieleweki ipasavyo kwa watumiaji na watekelezaji na wasifu wa walimu na wanafunzi haujafafanuliwa kwa uwazi."

"Sera haitoi mwongozo wa unyumbufu unaoruhusu elimu na mafunzo kupatikana kwa njia mbalimbali mbadala, uchambuzi wa kina wa sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014, masuala muhimu, changamoto na mapendekezo."

Pia, ripoti hiyo ilionesha kuwa muundo wa elimu unaobainishwa kwenye sera hiyo si nyumbufu na haitoi fursa mbadala za kujifunza, kutokuwapo na ufafanuzi wa tamko la matumizi ya lugha zote mbili za Kiswahili na Kiingereza kama lugha za kufundishia kwa ngazi zote za elimu kumechangia kuwapo kwa mkanganyiko kwenye tafsiri na utekelezaji wake na haitoi mwongozo kuhusu ukuzaji wa elimu ya uraia kwenye ngazi zote za elimu.

**"Sera haijatamka lengo kuu na malengo ya elimu ya kitaifa kwa kila sekta ndogo ya elimu, imetoa tamko la ujumla katika kushughulikia sekta ya elimu badala ya kutoa matamko mahususi yanayolenga sekta ndogo ndogo za elimu, imekosa mkakati wa utekelezaji na msukumo wa kisheria," alisema Dk. Meena.**



HABARI KITAIFA

# 'Vijana tumieni fursa za elimu'

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (CCM) (pichani), amewataka vijana nchini kuzitumia vizuri fursa za masomo zinazotolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili wapate elimu na kujiajiri kupitia taaluma zao.

Abood alitoa rai hiyo wakati wa mahafali ya kidato cha sita ya Shule ya Ngunya Open yaliyofanyika mjini hapa.

Mbunge huyo alisema serikali inafahamu vikwazo vilivyopo kwa vijana ikiwamo ajira na ndiyo maana imekuwa ikitoa nafasi za kuwasomesha elimu ya ufundi ili waitumie kujiajiri.

Abood alisema vijana wakiitumia vizuri nafasi ya elimu ya ufundi ambayo serikali inaisimamia, itawawezesha kujikwamua kiuchumi kwa kujiajiri na kuajiri wengine ambao katika kipindi hiki ambacho ulimwengu uko kwenye mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mkurugenzi wa Shule ya Ngunya, alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani ya kitaifa na kutoa wito kwa wazazi na walezi kutokata tamaa linapofika suala la kuwapeleka watoto shule.

Wanafunzi 143 wanatarajiwa kuhitimu kidato cha sita mwaka huu katika shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2014.

Katika hatua nyingine, Mbunge Abood alitoa Sh. milioni 3.5 kwa ajili Umoja wa Makanisa ya Mkoa wa Morogoro ili kusaidia kampeni inayoendeshwa na makanisa hayo inayofahamika kama 'Nitoke na Yesu' ambayo pia inahimiza uzalendo.



Akizungumza katika kampeni hiyo, Askofu mstaafu wa Kanisa Anglikana Tanzania, Donald Mtetemela, alisema moyo wa uzalendo unaendelea kukosekana katika kulipenda taifa pamoja na kuthamini vitu vinavyotokana na juhudi za watu wenyewe.

Askofu huyo alisema lengo la kampeni hiyo ni kuendelea kuisafisha mioyo ambayo imeanza kuondokewa na uzalendo, kukuza fikra za kizalendo kwa Watanzania na kujenga utamaduni wa kuthamini vitu vyao kwa faida yao na taifa.

# Shirika laomba sera kulinda watoto katika ajira isiyo rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake na Watoto (WLAC),kimeiomba serikali kutengeneza sera na sheria ambazo zitaweka ulinzi katika kundi la watu walio kwenye ajira isiyo rasmi nchini.

Akizungumza wakati wa kuadhimisha siku wa Wafanyakazi Duniani, Mwanasheria wa WLAC, Consolata Chikoti, alisema wanawake na vijana ndio kundi kubwa ambalo limekuwa likiangukia katika ajira zisizo na ulinzi na hivyo mara nyingi kujikuta likikosa kazi.

"Kaulimbiu ya siku wafanyakazi mwaka huu inasema 'maslahi bora, mshahara juu, kazi iendelee'. Serikali imeonyesha nia nzuri katika kusimamia maslahi ya wafanyakazi nchini hususani kupitia kaulimbiu hii ya mwaka huu," alisema Chikoti.

"Pamoja na nia hiyo nzuri ambayo serikali imeonyesha, lakini bado kuna kundi ambalo kila siku linakuwa linasahaulika. Kundi hili ni la watu waliopo katika sekta ya ajira isiyo rasmi, na ndilo lina watu wengi, likibeba wanawake na vijana.Hili ni la watu ambao wanafanya kazi kwa bidii sana lakini ajira zao hazina ulinzi."

"Wengi wao wanafanya kazi katika viwanda, wengine wanaajiriwa kama wapishi, wafanya usafi, wadada wa kazi kwenye majumba, kwa ujumla wao hili ni kundi muhimu sana ambalo linaonekana kusahaulika sana, lakini ni vema kwa sababu nalo linafanya kazi kama walivyo wafanyakazi wengine, wakapewa kipaumbele na wao hususani kwa kutengeneza sera na sheria ambazo zitalinda ajira zao."

Chikoti alisema kama WLAC na kama kituo cha wanasheria wabobezi, wamekuwa wakikupambana na idadi kubwa ya wafanyakazi katika kundi hilo kulalamikia kunyanyaswa na kutokutendewa haki na waajiri wao kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine.

"Na ndio maana katika sherehe za mwaka huu za wafanyakazi, sisi tumeamua kukutanisha kundi hili la wafanyakazi kwenye sekta isiyo rasmi ili na wao wajione kama wenzao na pia tutumie fursa hii kuwapa elimu ya kutambua haki zao mbalimbali na namna ya kuzipigania,"alisema Chikoti.

Alisema bado wanaamini kwamba serikali itahakikisha inaweka mazingira bora kwa kundi hilo kwa kuwa na wao wana mchango kwa nchi yao na ni walipa kodi kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine.

Diwani wa Kata ya Makumbusho, Mohammed Ally, alisema changamoto ya kutokuzingatiwa haki za wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi limekuwa ni la muda mrefu, na kwamba kuna haja ya kutafutiwa ufumbuzi.


brac

## TAARIFA KWA UMMA

Tunapenda kuuhabarisha umma kuwa kuna mtu asiyejulikana na mwenye nia ovu ambaye anatumia akaunti **FEKI** yenye jina la "Brac Maendeleo Tanzania" kuhadaa umma kuwa wanatoa mkopo kwa njia ya mtandao wa Facebook.

Hivyo tunatoa tahadhari kuwa akaunti hiyo ni feki na haina mahusiano yoyote na kampuni yetu na hivyo tunaomba wateja wetu na jamii kwa ujumla kupuuzia uzushi na ulaghai wa akaunti hiyo. Shirika dada letu la BRAC Maendeleo Tanzania, halitoi huduma ya mikopo bali limejikita katika kutekeleza miradi inayowawezesha watoto na vijana wa kike.

Tunawasihi wateja wanaotaka kupata huduma kutoka katika kampuni yetu, kufika katika matawi ya ofisi yetu.

Kwa mawasiliano zaidi, tupigie kwa simu namba 0800782206

Imetolewa na:

**Menejimenti**

**BRAC Tanzania Finance Ltd.**



twiga cement

HEIDELBERGCEMENTGroup

**TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY**

## TAARIFA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa wote wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka 2021 wa Wanahisa utafanyika kwa njia ya mtandao. TPC PLC inajali sana usalama kuliko mambo megine yote. Uamuzi wa kuufanya huu mkutano kwa njia ya mtandao ulifanyika ili kupunguza mikusanyiko ya watu na kulinda afya pamoja na usalama wa wanahisa wetu, wafanyikazi wetu, wakurugenzi wetu na washikadau wengine.

**Tarehe na Muda: Jumanne, tarehe 25 Mei, 2021, saa nne asubuhi**
**Uendeshaji Mkutano: Kwa njia ya mtandao, wenyeji wakiwa Chorus Call Africa**

**DONDOO**

1. Ufunguzi wa Mkutano: Katibu asome taarifa iliyotolewa kuuita Mkutano Mkuu na kuhakiki kama akidi ya Mkutano imetimia.
2. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 28 uliofanyika tarehe 28 Mei 2020.
3. Kupokea, kujadili na kama zitaafikiwa kupitisha taarifa ya wakurugenzi, taarifa ya wakaguzi na taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2020.
4. Kupokea, kujadili na kama litaafikiwa kuthibitisha gawio la mwaka 2020.
5. Kuthibitisha uteuzi wa wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Desemba 2021.
6. Kujadili mambo mengine ya kampuni ambayo taarifa zake zimepokelewa.

**Kwa Niaba ya Bodi**
**Tarehe: 3 Mei, 2021**

**Brian Kangetta**
**Katibu wa Kampuni**

1. Mwanahisa yeyote aliye na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, anaruhusiwa kuteua mwakilishi au wawakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Fomu ya kuteua mwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya kampuni (https://www.twigacement.com).
2. Mwakilishi atakayeteuliwa siyo lazima awe mwanahisa wa kampuni. Fomu ya kuteua mwakilishi ambayo imejazwa na mwanahisa inatakiwa iwasilishwe kwa CAD Securities Limited (kupitia anwani ya Barua Pepe: **judith@cadsecurities.com** au **neemak@cadsecurities.com** au utume picha ya fomu iliyojazwa kupitia Whatsapp [namba: +255 777 787 845]) angalau masaa 24 kabla ya muda wa kuanza mkutano, la sivyo fomu itakuwa haijakidhi vigezo.
3. Wanahisa wanaombwa kuwasiliana na CAD Securities Limited kupitia barua pepe tajwa au namba ya Whatsapp tajwa, ili kupata maelekezo zaidi kuhusu jinsi ya kushiriki kwenye Mkutano Mkuu.
4. Mahesabu kamili ya kampuni, ambayo yamepitishwa na wakaguzi, yanapatikana kwenye tovuti ya kampuni (**https://www.twigacement.com**).

HABARI KITAIFA

# DED Ikungi apewa tuzo ya mwajiri bora

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), mkoani Singida, kimempa tuzo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, kama mwajiri bora wa mwaka.

Tuzo hiyo iliolewa juzi wakati wa maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani kimkoa, na kukabidhiwa na Mkuu wa mkoa huo, Dk. Rehema Nchimbi.

Vigezo vilivyotumika kwenye tuzo hiyo ni mwajiri anayejali maslahi ya anaowasimamia, kutatua changamoto zao kwa kiasi kikubwa mwenye hofu na mcha Mungu katika utekelezaji wa majukumu ya umma kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuzi za utumishi.

Katibu wa TALGWU Mkoa wa Singida, Pandauyaga Ntulilah, alisema lengo ya kuanzishwa kwa tuzo hiyo ni kuwahamasisha waajiri kushirikiana kwa karibu na vyama vya wafanyakazi kwa kuhakikisha maslahi yao yanasimamiwa vyema.

"Tumetoa tuzo kwa vigezo vya mwajiri mwenye hofu ya Mungu, mlezi mzuri wa watumishi, msikivu na muwazi kwa watumishi wote bila ubaguzi na anayevitambua vyama vya wafanyakazi, kuitisha mabaraza ya wafanyakazi na kuwalipa posho zao hata angalau kidogo na kutatua migogoro ya wafanyakazi bila kuzalisha migogoro mingine," alibainisha.

"Ni muhimu waajiri wote wakatenda haki kwa watumishi, huku wakimtanguliza Mungu kama alivyofanya Kijazi," alisisitiza.

Akizungumza mara baada ya kupoka tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Ikungi, Kijazi alisema matatizo ya wafanyakazi yamegawanyika kwa kuwa kuna wafanyakazi wenye matatizo ya kijamii ambao wanahitaji mwajiri kuwasikiliza.

Alisema amejitahidi kujenga uhusiano bora kazini kwa kuhakikisha masuala ya kijamii kama msiba ambao wote hushiriki kwa umoja.

"Na ni kitu ambacho sikukitegemea lakini vile vile nimshukuru Mungu kwa kutuwezesha sisi kama Halmashauri ya wilaya ya Ikungi kutatua changamoto nyingi ambazo zilikuwa zikiwakabili wafanyakazi na kwamba umoja na mshikamano wetu ndiyo ambao umetusaidia kwa hiyo tuzo hii siyo ya kwangu mimi ni ya wafanyakazi wote,"alisema Kijazi.

Katika risala ya wafanyakazi iliyosomwa na Katibu wa TUGHE Mkoa wa Singida, Ethel Kahuluda, alizitaja baadhi ya changamoto zinazowakabili wafanyakazi hao ni waajiri wengi wa sekta binafsi kutojua sheria na mahusiano kazini,sheria ya mfuko wa fidia kwa wafanyakazi na sheria ya usalama mahali pakazi.

Nyingine ni ucheleweshwaji wa pensheni kwa wastaafu,baadhi ya wakurugenzi kutoitisha vikao vya mabaraza ya wafanyakazi kwa wakati,waajiri wengi wa sekta binafsi kutowasilisha makato yao ya asilimia kumi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, changamoto hiyo imewakumba pia wafanyakazi wa sekta binafsi na hivyo kuwafanya wasione umuhimu wa kujiunga na mifuko hiyo ya hifadhi ya jamii.

Mgeni rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Singda, Dk. Rehema Nchimbi, aliitaka TUICO kujenga utamaduni wa kutoa elimu kwa waajiri wa sekta binafsi ili waweze kufahamu juu ya umuhimu wa wafanyakazi wao kuwa na bima ya afya.

# Sababu maofisa ugani 1.500 kupewa pikipiki

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

Waziri wa Kilimo, Prof Adolf Mkenda, amesema serikali itawapa pikipiki maofisa ugani 1,500 ili kuwarahisishia kutoa huduma kwa wakulima na kuongeza tija na ufanisi katika sekta ya kilimo. Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea mashamba ya wakulima wa mtama katika Halmashauri ya Kongwa, mkoani Dodoma, Waziri Mkenda hakueleza kwa undani utaratibu utakuwaje, lakini alisema pikipiki zimeombewa fedha katika bajejti ya mwaka 2021//22 na kueleza kuwa hatua hiyo inatokana na dhamira ya serikali ya awamu ya sita ya kuikwamua sekta ya kilimo kwa kuwawezesha maofisa ugani, kufanya tafiti na kuhimiza matumizi ya mbegu bora ili tija katika kilimo iongezeke.

"Mkakati wetu kama wizara ni pamoja na kuwawezesha maofisa ugani ambao ni watu muhimu sana na ambao tunataka wawafikie wakulima katika maeneo yao. Moja ya mambo ambayo tutayafanya ni kuwapa pikipiki zitakazowawezesha kutoa huduma za kitaalamu kwa wakati," alisema.

Alisema wizara itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) ili kutafiti na kupata mbegu zinazokinzana na magonjwa pamoja na kuhimiza upimaji wa afya ya udongo ili kuleta tija kwenye kilimo. "Mbali na kuwawezesha maofisa ugani, serikali tunakusudia kufanya kazi na TARI, ambao wamejitahidi sana kuleta mageuzi ya mbegu bora na kupima afya ya udongo katika maeneo kadhaa nchini. Tunaamini kuwa uwapo wa mbegu bora, matumizi sahihi ya ardhi na uwezeshwaji wa maofisa ugani vitachangia sana kuleta mageuzi tunayoyahitaji," alieleza Waziri Mkenda.

Aliipongeza kampuni ya uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa bia (TBL) kwa makubaliano na wakulima ya kulima mtama katika Halmashauri ya Kongwa na kusema hatua hiyo inawahakikishia wakulima hao soko.

Mkulima wa matama katika eneo hilo, Michael Malima, alisifu mkataba huo na kusema unawahakikishia soko na kuongeza bei ya mtama wao. Alisema bei imepanda kutoka kati ya shilingi 200-300 kwa kilo na sasa ni shilingi 550 kwa kilo.




Mkurugenzi Mkuu wa shirika la Viwango Tanzania (TBS) Dkt. Athuman Ngenya akiongea wakati wa hafla ya uzinduzi wa mfumo wa mafunzo ya utayarishaji Viwango na udhibiti Ubora wa Bidhaa na huduma nchini kufanywa kwa njia ya Mtandao, uzinduzi huo ulifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Mifumo hii imebuniwa na TBS kwa kushirikiana na TradeMark East Africa (TMEA). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asakwa tuhuma za kumpa mtoto ujauzito mara mbili

**Na Mwandishi Wetu,**

PEMBA

MTOTO wa miaka 17 anadaiwa kupewa ujauzito mara mbili na shemeji yake katika Shehia ya Mchakwe Wilaya ya Mkoani Pemba.

Mama wa mtoto huyo alieleza kuwa kesi hiyo wameshaifikisha Polisi, ingawa wameambiwa wamtafute mtuhumiwa, jambo ambalo limekuwa gumu kwa upande wao.

Alisema jambo la kumkamata mtuhumiwa sio rahisi kwao, kwani amekimbia na hawamjui alipokwenda, ingawa wanasikia tetesi kuwa ameshafika Tanzania Bara.

"Hapa hayupo mara tunasikia yupo kwa Gombe hapa Muambe, mara yupo Unguja na wengine wanatwambia yupo Bara...kwa kweli hatujapata taarifa sahihi, hivyo hatujui tushike lipi, hata huyu mkewe hapa ameshahama," alisema mama huyo.

Alieleza mtoto wake kwa sasa ana ujauzito wa miezi saba, na kwamba alimgundua baada ya kumuona anatafuna mchele mara kwa mara, na alipomuuliza akamjibu kuwa ana ujauzito na amepewa na shemeji yake Mosi Othman Mosi (35).

Alisema, ana wasiwasi kesi hiyo imeshakwama kutokana na kutoulizwa chochote licha ya kuifuatilia, jambo ambalo linamuumiza sana kwani mtuhumiwa huyo ameshampa ujauzito mara mbili.

"Mwanangu hana damu hata kidogo licha kuwa na ujauzito wa miezi saba, na pia mtoto wake ni mgonjwa kwa sababu hana lishe bora, hivyo saa zote hayupo sawa," alieleza mama huyo.

Alisema, ameathirika sana kiafya na kiali, kwani aliumwa homa kali na hawezi hata kula, jambo hilo linamsababishia kushindwa kufanya shughuli zake ikiwamo za kilimo, kwani anapotembea anahisi kizunguzungu muda wote.

Akizungumzia ujauzito wa mwanzo wa mtoto wake, alisema, alijifungua mtoto wa kike wakati huo akiwa na miaka 15, ingawa hakufikia kumuachisha ndio akapata ujauzito mwingine akiwa na miaka 17.

"Mwanangu alipopata ujauzito wa kwanza alikuwa darasa la nne na hakuendelea tena, mtoto hajafika miaka miwili amebeba mimba nyingine, inaniuma sana, lakini yote ni kwa sababu mtuhumiwa aliachiwa," alieleza mama huyo.

Baba wa mtoto huyo alisema ujauzito wa kwanza wa mtoto wake, aliwataja watuhumiwa wawili ambao ni Mosi Othman Mosi na Suleiman Zahor Makame, ambao waliachiliwa.

Mjumbe wa Sheha ya Mchakwe, Khatib Hamad Vuai, alisema wamepokea taarifa hiyo.

Alisema kuwa, wanapopata taarifa za matukio ya udhalilishaji wanashirikiana na familia iliyoathiriwa, ingawa kesi zinapofika kituo cha Polisi, baadhi yao hawazishughulikii inavyotakiwa.

Alivishauri vyombo vya sheria kuchukua hatua kali kwa watendaji wa makosa hayo, ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Aliekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Ahmed Khamis Makarani, alisema, wamepokea taarifa hiyo, na kwamba wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Alisema kuwa, pia wanaendelea kumtafuta mtuhumiwa huyo na akipatikana atafikishwa mahakamani.




Wafanyakazi wa Tanzania Breweries Ltd Plc wakishirikia katika maadhimisho ya Mei Mos yaliyofanyika katika vuwanjwa wa Uhuru ijijini Dar es Salaam.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KMKM yakamata sukari ya magendo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

VIROBA 50 vya sukari vimekamatwa na kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) Wilaya ya Mkoani katika Bandari ya Makombeni.

Akizungumza na askari wa KMKM katika eneo la tukio, Mkuu wa Wilaya hiyo, Issa Juma Ali, alikipongeza kikosi hicho kwa kufanikiwa kukamata bidhaa hiyo ambayo ilikuwa inataka kusafirishwa kwenda kuuzwa nje ya kisiwa cha Pemba.

Alisema, amekuwa akipokea taarifa hizo kwamba kuna watu wanaofanya biashara hiyo haramu, na kwamba bidhaa hiyo itaifishwe.

Alisema baada ya kupokea taarifa ya uwapo wananchi wanaofanya biashara haramu ya magendo, Serikali kupitia kamati yake ilianza kufanya doria katika maeneo ya bandari hasa muda wa kufutari, kwani ndio wanaoutumia katika kufanya shughuli hizo.

"Tangu kuanza mwezi wa Ramadhani tumepokea taarifa mara tatu, lakini tuikuwa tunawakosa watu hawa, ila sasa wamenasa kwenye mtego wetu kwani siku za mwizi ni arobaini, hivyo watachukuliwa hatua za kisheria," alisema. Aliwataka watu wanaojihusisha na biashara hizo haramu, kuacha mara mija, kwani wanaikosesha serikali mapto yake.

Nae Mkuu wa kituo cha KMKM Wilaya hiyo, Luteni Abdi Mrisho Mahamuod, alisema majira ya mchana alipokea taarifa kutoka kikosi chake kilichopo Makombeni kuwa wakiwa kwenye doria za kawaida walifanikiwa kukamata bidhaa ambayo wanataka kuisafirishwa kwa njia ya magendo ambayo kupelekwa Tanga na ndipo walipofanya upekuzi wakagundua kuwa ni sukari.

Alisema baada ya jahazi kupandishwa juu walikuta polo 50 za sukari zilokuwa kwenye chombo hicho pamoja na kitanda kimoja aina ya banco.

# Usajili leseni biashara BRELA sasa siku moja

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAKALA wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA) umesema hivi sasa usajili wa leseni ya jina la biashara na leseni ya biashara vinapatikana ndani ya siku moja.

Hiyo inatokana na maboresho makubwa ya mifumo ya wakala ambayo yamelenga kuhakikisha wafanyabiashara wanarasimilisha biashara zao haraka.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Usajili wa wakala Gabriel Girangay, kwenye ufunguzi wa maonyesho ya ya Biashara, Uwekezaji na Utalii, katika viwanja vya Rock City Mall jijini hapa.

Girangay alisema BRELA imeboresha huduma inazotoa kwa wadau wake ikiwa ni pamoja na kupunguza muda wa kukamilisha usajili kwa kadri inavyowezekana lakini pia kuwahudumia wateja wote kwa ukaribu kupitia kituo cha miito.

"Kwa sasa muda wa usajili wa Jina la biashara ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi, usajili wa kampuni ni siku tatu na si zaidi ya siku tano za kazi. Usajili wa Alama za Biashara na huduma ni kipindi cha siku tisini kutokana na takwa la kisheria," alisema.

"Maombi ya kupata Hataza ni siku mia moja na ishirini (120) (kutokana na takwa la kisheria), kupata Leseni ya Kiwanda au Leseni ya Biashara kundi A ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi," alisema.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alielezea kufurahishwa kwake na hatua iliyofikiwa na (BRELA) katika kupunguza urasimu.

Akizungumza kenye ufunguzi wa maonesho hayo, Ndaki aliwataka wafanyabiashara na wajasiriamali wa Mkoa wa Mwaza kutumia fursa ya uwepo wa BRELA katika maonesho haya kutatua changamoto zao na kupata elimu.

"Changamoto zinazosemekana zipo katika urasimishaji biashara sasa ndio muda wake kuzimaliza na bahati nzuri BRELA wapo katika maonesho haya, fikeni katika banda lao la maonesho, pateni elimu, wasilisheni changamoto zenu hapo na rasimisheni biashara papo kwa hapo," lisema Mhe. Ndaki.

Girangay alisema BRELA inashiriki maonesho haya ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa kuwafikia wadau wake katika maeneo yao kwa lengo la kuwapa elimu juu ya umuhimu wa kurasimisha biashara.

Alisema wanaelimisha pia kuhusu, taratibu za urasimishaji biashara na gharama zake, kutatua changamoto na kufanya usajili wa papo kwa hapo.

Maonesho ya Biashara Uwekezaji yaliyoandaliwa na Rock City Mall yalifanyika kwa siku tatu kuanzia Aprili 30 na kumalizika jana.

# Watendaji kata waagizwa kutoa taarifa za mapato

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya Kibaha mkoani Pwani, Erasto Makala, amewaagiza watendaji wa kata kuhakikisha wanatoa taarifa za mapato na matumizi kwenye taarifa za kata wanazoziandaa kwa ajili ya baraza la madiwani.

Makala alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha baraza la madiwani kujadili taarifa za kata kilichofanyika Mlandizi.

Alisema kwenye kata kuna makusanyo yanafanyika, lakini taarifa ya kinachopatikana na matumizi yake hakijawahi kutolewa taarifa.

" Fedha zote hizo zinazokusanywa ni za umma zijulikane zinazoingia na kutoka, ziainishwe kwenye taarifa za kata ili baraza lijue kinachofanyika kama kuna sehemu ya kutoa ushauri madiwani tufanye hivyo," alisema.

Hata hivyo, katika mikakati ya kuinua makusanyo ya Halmashauri hiyo imeunda kikosi kazi kinachokusanya mapato, lengo likiwa ni kuziba mianya ya upotevu wa mapato na kuinua kiwango cha ukusanyaji.

Aidha, Makala ambaye pia ni diwani wa Magindu, alisema katika kata hiyo wamekuwa wakiwahamasisha wananchi kujitolea kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili fedha ambazo.zingelipa kwa kazi ambazo wanaweza kuzifanya zipelekwe kufanyia vitu vingine. Alisema endapo kila kata itaweka utaratibu huo, itasaidia kupunguza tofauti katika sekta mbalimbali kwa kutumia kiasi cha fedha kinachotolewa kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Naye Diwani wa Soga, Shomari Minsheshe, alieleza katika baraza hilo kuwa unahitajika ushirikiano kati ya Serikali na wazazi kuwahimiza wanafunzi kuhudhuria shule, kwani katika kata hiyo bado kuna hali ya utoro kwa wanafunzi wa kidato cha pili na kidato cha kwanza kutoripoti kwa wakati.

Alisema utoro katika kata yake bado upo, hivyo kusisitiza ushirikiano ili kuukomesha na watoto wahudhurie vipindi vya masomo pamoja na kuinua kiwango cha ufaulu katika halmashauri hiyo.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WANAOLIPWA MKWANJA MREFU ZAIDI SERIE A UK. 12-13



# NYOTA WA5 MGUU WA KULIA KAMA WA KUSHOTO

SON

## ISIKUPITE

TANGU Pep Guadiola ajiunge na Manchester City miaka mitano iliyopita (2016) Manchester City wamefunga mabao mengi kuliko timu yoyote kutoka Ligi Kuu England katika michuano yote (mabao 700), ambayo ni 157 zaidi ya timu inayofuatia Liverpool yenye mabao 543 huku Tottenham ikifuiata na mabao 532, Arsenal (522), Chelsea (515), Man United (512) na Leicester (371).



**LONDON,** England

MWANASOKA wa kisasa, anakuwa na uwezo wa vitu vingi, licha ya nafasi yake uwanjani, anakuwa na uwezo wa kufunga, kupiga chenga na pasi za mabao.

Lakini wakati mwingine inakuwa vigumu kwa mchezaji kufanya vitu vyote kwa wakati mmoja kutokana na nafasi anayocheza dimbani.

Wachezaji kama Ronaldinho na Maldini wanachukuliwa kama wachezaji bora zaidi waliokuwa wanatumia miguu yote miwili kwa ufasaha kabisa wakiwa dimbani.

Ni mara chache sana kumkuta mchezaji akiwa na uwezo wa kutumia miguu yote miwili kwa ufanisi mkubwa.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watano ambao wana uwezo mkubwa wa kutumia miguu yote miwili, twende sasa...

### #5. MASON GREENWOOD | MANCHESTER UNITED

Huyu ni kinda wa Manchester United, Mason Greenwood ambaye amejiimarisha yeye mwenyewe kwenye safu ya ushambuliaji ya United akifananishwa na Robin van Persie.

Tangu kuanza kwake katika msimu wa 2018-19, Greenwood kwa haraka zaidi amepaa kwenye kiwango cha juu. Kupanda kwenye kikosi cha kwanza kulikuwa baada ya kumaliza msimu akiwa mfungaji bora wa kikosi cha wachezaji chini ya umri wa miaka 18, akitikisa nyavu mara 17 kwenye msimu wa 2017/18.

Baada ya kutamba kwenye timu za vijana, Greenwood amekuwa akicheza mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza. Mara ya kwanza ilikuwa chini ya kocha, Jose Mourinho mwaka 2018, kabla ya kuanza vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSG.

Greenwood ana uwezo wa kucheza kwa kutumia miguu yote miwili katika kupiga mashuti na chenga.

Amehusika kwenye mabao 36 (Mabao 26, pasi za mwisho kumi) kwenye mechi 97. Greenwood bila shaka yoyote ndiye mchezaji wa Manchester United mwenye uwezo wa kutumia miguu yote miwili kwa ufanisi mkubwa zaidi.

### #4. OUSMANE DEMBELE | FC BARCELONA

Mchezaji mwingine kijana ni Ousmane Dembele - ambaye ana uwezo wa kutumia miguu yote miwili. Raia huyo wa Ufaransa alihamia kwenye dimba la Camp Nou baada ya kutumia msimu mmoja tu kule Borussia Dortmund. Dembele alitua Dortmund akitokea Nice kwa pauni milioni 13.5 kwenye uhamisho wa mwaka 2016 na mwaka mmoja baadaye ada yake ikagharimu kiasi cha pauni 121.5.

Ingawa maisha ya Dembele pale Catalunya yamekuwa ya kupanda na kushuka, lakini msimu huu unaonekana kuwa bora zaidi kwake.

Wakati alifunga mabao 22 kwa msimu wa kwanza kuichezea Barcelona, mabao 12 alifunga kwa mguu wa kushoto na kumi kwa mguu wa kulia.

### #3. CRISTIANO RONALDO | JUVENTUS

Mmoja wa wachezaji bora kabisa kwenye soka la kisasa, Cristiano Ronaldo na amefunga mabao mengi sana kwa mguu wake wa kushoto. Katika mabao yake 700 kwenye soka la ushindani, 442 amefunga kwa mguu wa kulia na 129 kwa mguu wa kushoto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, amefunga mabao 127 kwa kichwa. Na Ronaldo anaendelea kufanya vizuri kule kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Raia huyo wa Ureno anaongoza kwenye orodha ya wafungaji kwenye Ligi Kuu ya Italia, msimu huu 2020/21 akiwa na mabao 25. Hivi karibuni alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 50 kwenye ligi tatu kati ya tano kubwa za Ulaya (Ligi Kuu England, LaLiga na Serie A).

Zaidi ni kwamba amefunga mabao mengi zaidi kwa msimu mmoja pale Juventus (msimu wa 2019-20) - akicheka na nyavu mara 87.

### #2. IVAN PERISIC | INTER MILAN

Ivan Perisic ni mmoja wa mawinga bora kabisa barani Ulaya kwa kipindi cha miaka kadha sasa.

Perisic anajulikana kwa uwezo wake wa kupiga krosi nzuri kutoka pembeni ya uwanja. Raia huyo wa Croatia amekuwa kwenye wakati bora zaidi katika Klabu yake ya Inter Milan tangu ajiunge nayo.

Jose Mourinho alikuwa shabiki mkubwa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 na alipambana kutaka kumpeleka pale Old Trafford, kwa ajili ya kumlisha mipira straika wa wakati huo Zlatan Ibrahimovic, ambaye alikuwa akicheza hapo.

### #1. SON HEUNG-MIN | TOTTENHAM HOTSPUR

Son Heung-Min ni mmoja wa mawinga bora zaidi barani Ulaya kwa sasa na amekuwa na wakati wa kuvutia kule kwenye Ligi Kuu England, akikipiga pale Tottenham Hotspur.

Raia huyo wa Korea Kusini amekuwa na uwezo mkubwa wa kutumia miguu yake yote miwili kama ilivyo kwa Greenwood, Dembele na Ronaldo.

Nje ya mabao yake 67 kwenye Ligi Kuu England aliyoifungia Spurs, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ametupia mabao 37 kwa mguu wa kulia na 26 kwa 'guu' lake la kushoto na manne kwa kichwa. Kipindi alichocheza kule Bayer Leverkusen, Son alifunga mabao 13 kwa mguu wake wa kulia na 12 kwa guu la kushoto.

# WACHEZAJI 10 WANAOLIPWA MKWANJA MREFU ZAIDI SERIE A



IBRAHIMOVIC

**ROME,** Italia

SERIE A ni moja ya ligi tano kubwa barani Ulaya na inapambwa na baadhi ya wachezaji bora duniani, kama vile Cristiano Ronaldo. Ligi hiyo Kuu ya Italia pia inawajumuisha wachezaji wenye vipaji vikubwa duniani, katika klabu kubwa kama Juventus, Inter Milan na AC Milan.

**Juventus ni moja ya klabu zinazotumia fedha nyingi zaidi kwenye usajili wa wachezaji, na kwa sasa bili yao ya mishahara kwa mwezi inakaribia pauni milioni 213.**

Ingawa nyota wa Bianconeri ni kati ya wachezaji wanaolipwa zaidi kwenye ligi hiyo, lakini pia wachezaji wengine wanaotoka katika klabu za Inter Milan, Napoli na Roma ni miongoni mwao.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 wanaolipwa mishahara mikubwa zaidi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, hawa hapa...

### #10. ALEXIS SANCHEZ (INTER MILAN) – PAUNI 225,000 KWA WIKI

Mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Alexis Sanchez, ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa zaidi kwenye Serie A. baada ya mwaka mmoja wa mkopo na Inter Milan, alisaini mkataba wa miaka mitatu wa kuendelea kukaa na timu hiyo, kuanzia msimu huu.

Sanchez anabeba nyumbani kiasi cha pauni 225,000 kwa wiki ambacho pia alikuwa akilipwa kule Man United.

Hata hivyo, hajaweza kuwa kwenye kiwango chake bora kama alivyokuwa wakati akicheza Arsenal kwa misimu kadhaa. Kwa jina lake amefunga mabao 45 na ndiye anayeongoza kwa wafungaji bora kwenye kikosi cha Chile.

### #9. ADRIEN RABIOT (JUVENTUS) – PAUNI 225,000 KWA WIKI

Mchezaji wa kwanza wa Juventus kwenye orodha hii ni Adrien Rabiot. Kiungo huyo alijiunga na 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kipindi cha majira ya joto mwaka 2019 kwa uhamisho huru akitokea Paris Saint-Germain.

Kiungo huyo raia wa Ufaransa kwa sasa analipwa kiasi cha pauni 225,000 kwa wiki.

### #8. AARON RAMSEY (JUVENTUS) – PAUNI 225,000 KWA WIKI

Aaron Ramsey alijiunga na Juventus kwa uhamisho huru msimu wa 2019-20, na anachukua kiasi cha pauni 225,000 kwa wiki.

Kiungo huyo wa zamani wa Arsenal amekuwa hapati sana nafasi ya kucheza pale kwenye dimba la Allianz kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu iliyopita. Ameshindwa kujiimarisha yeye mwenyewe kwenye kikosi cha kwanza kwa miamba hao wa Serie A.

Ramsey amecheza mechi 11 za Serie A msimu huu na alifungua akaunti yake ya mabao msimu wa 2020-21 wakati Juve ikishinda mabao 3-1 dhidi ya Sassuolo.

### #7. ZLATAN IBRAHIMOVIC (AC MILAN) – PAUNI 225,000 KWA WIKI

Straika huyu wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic katika umri wake wa miaka 39, bado anaendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia kabisa, akiwa amefunga mabao 10 kwenye Serie A katika mechi saba alizocheza.

Mara nyingi wachezaji wa umri wake huwa wanamalizia soka lao kwenye Ligi Kuu Marekani, MLS, lakini yeye anatamba kule Serie A, akiwa anachukua nyumbani kiasi cha pauni 225,000 kwa wiki.

### #6. PAULO DYBALA (JUVENTUS) – PAUNI 230,000 KWA WIKI

Paulo Dybala anatambulika kama mmoja wa wachezaji wenye kipaji cha ukweli kwenye Serie A, hivyo haishangazi kumuona akitamba kwenye jezi za Juventus.

Straika huyo ambaye alijiunga na Juventus mwaka 2015 akitokea Palermo, amefunga mabao 70 kwenye Serie A kwa klabu yake tangu awasili. Wakati akiwa anasuasua katika mechi za hivi karibuni, alitajwa kuwa mchezaji mwenye thamani kubwa wa Serie A (MVP) msimu wa 2019-20 na mshahara wake ni pauni 230,000 kwa wiki.

### #5. EDIN DZEKO (AS ROMA) – PAUNI 240,000 KWA WIKI

Straika wa AS Roma, Edin Dzeko ni mmoja wa wachezaji wachache ambao wamekuwa wakipata mshahara mkubwa zaidi kwenye timu yake.

Mshahara wake wa pauni 240,000 kwa wiki unaonekana kama ni mkubwa mno kutokana na ukweli kwamba anafikia katika kipindi chake cha mwisho cha uchezaji. Hata hivyo, Dzeko ni mchezaji muhimu kwa AS Roma na amefunga mabao saba katika mechi za ugenini 14 msimu huu.

### #4. ROMELU LUKAKU (INTER MILAN) – PAUNI 250,000 KWA WIKI

Washambuliaji mara zote ndio wachezaji wanaolipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha kwenye timu ya mpira wa miguu.

Usajili wa Romelu Lukaku wa pauni milioni 74 mwaka 2019, ulionekana kama kamari kwa kocha Antonio Conte. Bahati nzuri kwake umelipa na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa akifunga mara kwa mara.

Kwa sasa anapokea kiasi cha pauni 250,000 kwa wiki kama mshahara wake, ukiwa ni sawa na ule aliokuwa akilipwa kwenye klabu yake ya zamani ya Manchester United.

### #3. CHRISTIAN ERIKSEN (INTER MILAN) – PAUNI 250,000 KWA WIKI

Inter Milan imesajili wachezaji wengi wapya kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita. Baadhi ya wachezaji waliosajiliwa ni Ashley Young, Lukaku, Achraf Hakimi, na Arturo Vidal na wamekuwa na mwanzo mzuri kwenye Serie A.

Christian Eriksen, ambaye alisajiliwa kwa mkataba wa miaka mine na nusu na Nerazzurri Januari mwaka jana, anabakia kuwa wa aina yake. Hata hivyo, kiungo huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur, ameshindwa kuwa kwenye kiwango bora. Anapokea mshahara sawa na Lukaku, lakini kiwango chake dimbani kipo mbali sana na raia huyo wa Ubelgiji.

Afisa Mtendaji wa Inter, Giuseppe Marotta alithibitisha mwezi uliopita kwamba, Inter inaangalia uwezekano wa kumuuza Eriksen ambaye anapokea mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki, kipindi cha majira ya joto.

### #2. MATTHIJS DE LIGT (JUVENTUS) – PAUNI 280,000 KWA WIKI

Matthijs de Ligt, ni mlinzi mwenye umri wa miaka 21, kwa sasa ndie anashika nafasi ya pili kwa wachezaji wanaolipwa mkwanja mrefu zaidi kwenye Serie A. ni nadra sana kukuta mchezaji wa safu ya ulinzi akiwa kwenye orodha ya wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa. Lakini raia huyo wa Uholanzi ameweza kupenya mara baada ya kutua hapo akitokea Ajax.

Matthijs de Ligt alikosa muda mwingi wa kucheza kwa mwaka 2020 kutokana na kusumbuliwa na majeraha, lakini sasa yuko fiti.

Mshahara wake wa sasa ni pauni 280,000 kwa wiki na inaonekana wazi kuwa De Ligt ana muda mwingi zaidi wa kucheza kutokana na umri wake.

### #1. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS) – PAUNI 520,563 KWA WIKI

Cristiano Ronaldo ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye Serie A. mshahara wake ni pauni 520,563 kwa wiki.

Hata hivyo, kiasi hicho cha Ronaldo ni nusu tu ya mshahara anaochukua mpinzani wake, Lionel Messi kule Barcelona. Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, haonyeshi ishara yoyote ya kushuka kwa kiwango chake, hivyo bado ana nafasi ya kuendelea kucheza zaidi.

## Nukuu

"Ninajaribu kufurahia mpira wa miguu, unajua, nadhani nataka kuwa kocha, kwa kweli, ningependa kuwa mkufunzi. Sijui ni timu gani ningependa kusimamia. Kwa kweli, timu kubwa ikiwa nitaweza kuisimamia Manchester United, nitafurahi," **Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes.**



"Kylian [Mbappe] anapenda soka, anapenda kuzungumzia kuhusu soka, anaulizia kuhusu England – mchezo ukoje, tamaduni zao zikoje pale? – na pia anaulizia kuhusu Hispania na Argentina. Anatazama kila siku mechi za England, Ufaransa, Italia na Ujerumani," **Kocha Mkuu wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino.**



"Karim ni mchezaji wa aina yake nina furaha kuwa naye, lakini sishangazwi kwa kile anachofanya katika kila mchezo. Hali ni sawa kwa wachezaji wangu wote. Nina furaha kwa wachezaji wote, tunajua kwamba tunakwenda London [dhidi ya Chelsea] na tunatakiwa kufunga mabao ili tuweze kufuzu fainali ya Ligi ya Mabingwa," **Kocha Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane.**





Kiungo mshambuaji wa Simba, Luis Miquissone akijaribu kuwatoka wachezaji wa Yanga, Tuisila Kisinda (Kulia) na Farid Mussa, huku Michael Sarpong akiangalia kama anaweza kwenda kutoa msaada, kwenye mechi ya 'dabi' Novemba 7, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa mechi ikimalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MAKTABA**

# USIYOYAJUA 'DABI' SIMBA NA YANGA JUMAMOSI HII

**Na Adam Fungamwango**

MACHO na akili za mashabiki wa soka nchini sasa zimeelekezwa kwenye mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga utakaocheza Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Ingawa timu hizo zinatumia uwanja mmoja, Simba ndiyo itakuwa mwenyeji wa mechi hiyo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu iliyochezwa Novemba 7, mwaka jana katika uwanja huo huo timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

Yalikuwa ni mabao ya Michael Sarpong kwa mkwaju wa penalti dakika ya 31 na Joash Onyango dakika nne kabla ya mechi kumalizika.

Timu hizo zinakwenda kukutana huku Simba ikiwa inaongoza kwenye msimamo wa ligi, ikiwa na pointi 61, wakati Yanga ikiwa kwenye nafasi ya pili kwa pointi 57.

Hata hivyo, Simba ina michezo miwili pungufu ya Yanga, ikiwa imecheza mechi 25 na watani zao wa jadi 27 na hata mechi hiyo iikichezwa, bado Mabingwa Watetezi watakuwa wana michezo miwili ya ziada.

Ingawa kwa sasa Simba inaonekana iko vizuri zaidi, lakini kama kawaida ya mechi za watani wa jadi huwa haziamuliwi na uzuri wa kikosi, bali na mbinu na jinsi wachezaji watakavyojitoa kwa asilimia nyingi siku hiyo.

## TIMU ZOTE MAKOCHA WAPYA

Mechi hiyo itachezwa huku timu zote zikiwa na makocha wapya. Makocha wote hao wametoka kwenye timu moja ya Al Merrikh ya Sudan, mmoja akiwa amevunja mkataba na mwingine kutimuliwa.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes da Rosa, alijiunga na klabu hiyo Januari mwaka huu baada ya kuvunja mkataba na timu hiyo maarufu nchini Sudan, huku Kocha Mkuu wa Yanga Mtunisia, Nasreddine Nabi akijiunga katikati ya Aprili.

Nabi, aliyechukua nafasi ya Gomes, alijiunga na Yanga akiwa ametimuliwa na Al Merrikh baada ya kutofanya vema kwenye michuano Ligi ya Mabingwa Afrika, na ni muda mfupi tu baada ya suluhu dhidi ya Simba nchini Sudan.

Makocha wote hao wanachukua nafasi za Sven Vandenbroeck kwa upande wa Simba na Cadric Kaze wa Yanga ambao ndiyo waliozionGoza timu hizo kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

## 'MZEE WA KUKERA' ATAKUWAPO

Kwa mara ya kwanza huenda Simba ikamtumia mchezaji Benard Morrison kwenye mechi ya Mei 8, baada ya kukosekana katika mchezo wa mzunguko wa kwanza alipokuwa anatumikia adhabu ya kutocheza mechi tatu.

Mghana huyo ambaye alizua gumzo kwenye usajili wake kabla ya msimu huu kuanza na baadaye kuidhinishwa kuichezea Simba akitokea Yanga, aliifungiwa mwishoni mwa Oktoba mwaka jana kwa kosa la kumpiga ngumi Juma Nyosso kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting, hivyo aliikosa mechi ya Novemba 7, mwaka jana. Kama kocha Gomes atamtumia, basi itakuwa ni mara ya kwanza kwa Morrison kucheza dhidi ya waajiri wake wa zamani Yanga.

Ikumbukwe mchezaji huyo ndiye aliyeipa ushindi Yanga kwa mara ya mwisho ilipoifunga Simba bao 1-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa, Machi 8, mwaka jana.

## 'MAPRO' KUENDELEA KUTAMBA?

Mara ya mwisho kwa Watanzania kufunga mabao kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa Januari 4, mwaka jana, kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu msimu wa 2019/20.

Wachezaji hao wote ni wa Yanga. nao ni Mapinduzi Balama na Mohamed Issa 'Banka', kwenye mechi ambayo timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2, yote ya Simba yakifungwa na wageni, Mnyarwanda Meddie Kagere na Mkongomani Deo Kanda.

Baada ya hapo Morrison aliipa ushindi Yanga wa bao 1-0 kwenye mechi ya mzunguko wa pili, huku msimu huu mechi ya mzunguko wa kwanza Mghana mwingine Sarpong akiifungia Yanga na Mkenya akiisawazishia Simba kwenye sare ya bao 1-1. Je safari hii Watanzania watafunga mabao kwenye 'dabi' hii?

## WAZOEFU WA 'DABI' HAWA HAPA

Baadhi ya wachezaji ambao kama watapangwa basi watakuwa hawana presha sana kutokana na kuzoea kucheza mechi hizo.

Wachezaji nao kwa upande wa Simba baadhi yao ni Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', Paschal Wawa, Jonas Mkude, Hassan Dilunga, Kagere, na Erasto Nyoni. Upande wa Yanga ni Metacha Mnata, Haruna Niyonzima, Feisal Salum 'Fei Toto', na Juma Makapu.

## DABI YA LIGI KUU MARA YA KWANZA


Kuna baadhi ya wachezaji watakuwa wanaigusa 'dabi' ya Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, achana na ile ya fainali ya Kombe la Mapinduzi.

Wachezaji hao ni Saido Ntibazonkiza na Fiston Abdulrazack wa Yanga, kwa upande wa Simba kukiwa na Thadeo Lwanga na Parfect Chikwende.

Saido na Lwanga wameshawahi kuonja joto ya mechi ya watani, kwani walikuwapo kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi, lakini Chikwende na Fiston wao watakuwa wakigusa dabi hiyo kwa mara ya kwanza kama wakipangwa.

Wachezaji hawa wote walisajiliwa kwenye kipindi cha dirisha dogo.

**JE, WAJUA?**



NI Lionel Messi mabao 36 na Cristiano Ronaldo (35) pekee, ndio wachezaji wamefunga mabao mengi zaidi dhidi ya timu tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Karim Benzema akifuata na mabao yake 33, sawa na Raul.





# Watumishi wa umma watakiwa kutambua afya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATUMISHI wa umma wametakiwa kujenga tabia ya kutambua afya zao mara kwa mara, kutokana na asilimia 60 ya watumishi kuonyesha wana tatizo la uzito kupindukia na msongo wa mawazo.

Daktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Dk. Garvin Kweka, alibainisha hayo jana kwenye mafunzo pamoja na upimaji wa afya kwa watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Alisema mafunzo yanalenga kuzungumza na watumishi ili kuwasaidia kujenga tabia ya kutambua afya zao mara kwa mara.

"Leo nimekuja kuzungumza na watumishi hawa kwani tumekuwa tukipoteza nguvu kazi nyingi kutokana na magonjwa, asilimia 60 ya watumishi inaonesha wana tatizo la uzito kupindukia pamoja na msongo wa mawazo... kwa hiyo mafunzo haya yatawasaidia kutambua nini wafanye na kipi wasifanye ili kuwa na afya njema kuendelea kuleta tija katika maeneo yao ya kazi," alisema Dk. Kweka.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Kaimu Katibu Mkuu wa Sekta ya Mifugo, Prof. Hezron Nonga, aliwataka watumishi hao kupima afya kama ambavyo muongozo wa kudhibiti Virusi vya Ukimwi (VVU), Ukimwi na magonjwa sugu yasiyoambukiza mahala pa kazi unavyowataka.

Alisema upimaji wa afya kwa watumishi wa umma kwa mujibu wa muongozo huo wa mwaka 2014 ni jambo la lazima sio hiari, na kwamba itasaidia kubaini matatizo waliyonayo na kuwashirikisha waajiri wao ili kupata msaada.

Prof. Nonga alisema kwa mtumishi ambaye atabainika baada ya vipimo kuwa ana maambukizi, taratibu zinamtaka mwajiri wake kumpatia kiasi cha Sh. 100,000 kila mwezi.

Akizungumzia mafunzo hayo, alisema kuwa wafanyakazi hao watapatiwa mada mbalimbali kutoka kwa watalaam wa masula ya afya.

Alisema pamoja na kuwataka wafanyakazi kupima afya zao pia wanatakiwa kutambua namna ya kuishi hasa katika kuzingatia masuala ya ulaji wa vyakula, unywaji wa pombe, uvutaji wa sigara.

Mratibu wa Ukimwi, VVU na magonjwa sugu yasiyoambukiza mahala pa kazi, sekta ya mifugo, Rachel Maliselo, alisema lengo la upimaji huo ni kutoa fursa kwa wafanyakazi kupima afya zao kwa mujibu wa muongozo huo.

# 'Wanawake, wasichana wenye VVU wanatengwa zaidi na jamii'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAWAKE na wasichana wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU), pamoja na watu wenye ulemavu ni makundi yanayotengwa kwa kiasi kikubwa na jamii.

Kutokana na hali hiyo, imedaiwa kuwa wanashindwa kupata huduma za msingi ikiwamo za kiafya na kielimu.

Mratibu wa Programu za Ukimwi na jinsia kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN-Women), Jacob Kayombo, alisema hayo kwenye mafunzo kwa viongozi wa halmashauri na mitandao ya makundi hayo, yaliyofanyika jijini hapa.

Mafunzo yameratibiwa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), kwa ufadhili wa mfuko wa Global kwa uwezeshaji kutoka UN-Women.

Kayombo alisema watu wanaoishi na VVU bado hawatambuliki na hata fursa zinazotolewa kwa makundi haziwafikii na wamekuwa wakijitegemea kwa shughuli ndogo na wakati mwingine kukosa nauli ya kusaidia kufuata huduma za afya.

"Bado kuna uhitaji mkubwa na washiriki wenyewe wametaja kwenye mafunzo vikwazo wanavyokumbana navyo, wameshauri kuwapo na ushawishi na mipango mizuri kuanzia ngazi halmashauri kutengeneza mipango inayojumuisha mahitaji yao," alisema.

Alifafanua kwa upande watu wenye ulemavu, wamekosa fursa ya kupata elimu kutokana na wazazi kutoona umuhimu wa kuwapeleka shule.

"Wametuambia walikuwa wamewekwa mateka ndani kutokana na familia kuona aibu kuwashirikisha mambo ya kijamii na kukosekana kwa uelewa katika jamii ndio sababu ya unyanyapaa dhidi yao," alisema.

Pia, alisema wapo kwenye hatua za mwisho kutengeneza mwongozo ambao utatumiwa na wadau katika udhibiti wa VVU kitaifa kwa mwelekeo wa kijinsia.

"Leo tumewakutanisha kinamama na wasichana wanaoishi na VVU pamoja na watu wenye ulemavu kutokana na kukabiliwa na tatizo kubwa kwa jamii la unyanyapaa na ni dhana ambayo tumekuwa tukizungumzia kwa muda mrefu, tumeangalia chanzo ni nini, mila, tabia, mitazamo katika jamii ambayo inajengwa na ile hali ya kukata tamaa na hali ya mtu," alisema.

Naye, Mratibu wa masuala ya jinsia kutoka TACAIDS, Judith Luande, alisema katika mafunzo hayo wanafundisha viongozi hao wa halmashauri kuhakikisha wanashuka kwenye kata na vijiji kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya Ukimwi kwa mtazamo wa kijinsia.

"Tunawawezesha kujua jinsi ya kupata haki zao za msingi ili kufikia huduma za VVU na Ukimwi, imeonekana watu wenye ulemavu na Ukimwi wanakosa kufikia huduma kutokana na kupata manyanyaso ya kijinsia," alisema.

Alisema wamekuwa wakikumbana na vikwazo katika kupata huduma zao za msingi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa nauli ya kuwafikisha kwenye maeneo ya kupata huduma, na kwa wale wenye ulemavu hawaruhusiwi kutoka nje ya nyumba au kutafuta huduma za kiafya.

Mmoja wa washiriki ambaye ni mtu mwenye ulemavu kutoka Bariadi, mkoani Shinyanga, Hoka Maduhu, alisema wazazi wake walikataa kumsomesha wakidai atachekwa shule kutokana na ulemavu wake, lakini baada ya kukaa kwa muda nyumbani aliamua kujipeleka shule.

"Nilijipeleka shule na nikahitimu darasa la saba, lakini matokeo hayakuwa mazuri, nilikaa miaka mitatu nyumbani sikupata mchumba kwa kuwa kila mtu alikuwa anasema hawezi kuoa mlemavu, nikabeba mimba siku ya kujifungua hospitali walinikataa wakasema hawawezi kuhudumia mlemavu nikarudi nyumbani kujifungua," alidai.

Magreth Masalu kutoka Bariadi Vijiji, alisema bado kuna unyanyapaa kwa jamii na kushauri elimu itolewe hasa vijijini kutokana na kutokuwa na uelewa namna ya kuishi na watu wenye VVU.



Wafanyakazi kutoka sekta mbalimbali za umma wakiimba wimbo wa mshikamano kwenye Maadhimisho ya Mei mosi yaliyofanyika mkoani Dodoma katika uwanja wa Jamhuri juzi. **PICHA PETER MKWAVILA.**

# Waajiri wasiotoa zawadi kwa wafanyakazi bora wapewa siku 4

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amekemea tabia za baadhi ya waajiri kutokutoa zawadi kwa wafanyakazi kwa visingizio vya mchakato kutokukamilika, huku akiwapa siku nne za kazi kukamilisha suala hilo.

Dk. Mahenge alitoa kauli hiyo juzi kwenye sherehe ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi).

Alisema baadhi ya waajiri wamekuwa wakionyesha picha mbaya kwa kutanguliza kutoa vyeti kwa wafanyakazi bora, lakini wanapofikia suala la zawadi ya fedha wanasema mchakato haujakamilika.

"Kutokana na hali hiyo, natoa siku nne kwa halmashauri ambazo hazijatoa fedha ya zawadi kwa wafanyakazi bora ikiwamo halmashauri ya Bahi ikamilishe mara moja," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, uongozi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini umetoa Sh. milioni 29.4, ikiwa kama motisha kwa watumishi wake kuanzia ngazi ya chini hadi Profesa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya sherehe hizo, Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Taaluma), Dk. Provident Dimoso, alisema hatua hiyo imetokana na uongozi kukubaliana na kutambua kuwa maendeleo ya chuo hicho yanatokana na ushirikiano wa viongozi na wafanyakazi.

Alisema fedha hiyo imetolewa kwa ajili ya watumishi wote 294 na kila mmoja atapata Sh. 100,000 kuanzia mhudumu wa ngazi ya chini hadi mkuu wa chuo bila kujali nafasi ya mtumishi.

Alisema utawala wa chuo hicho ulifikiria kutoa zawadi kwa wafanyakazi wote bila kubagua kwa kutambua wazi kwamba maendeleo ya chuo yanatokana na umoja, upendo na mshikamano kwa kila mmoja kutimiza majukumu yake kwa wakati.

"Unaweza kuona kuwa ndani ya miaka miwili ya nyuma chuo kilikuwa na wanafunzi 8,000, lakini kwa sasa wapo wanafunzi 15,000 kwa miaka miwili ya nyuma chuo kilikuwa na heka 60, lakini kwa sasa ni heka 700 ambazo chuo kimenunua kwa fedha taslimu na yapo magari mapya sita ikiwamo gari maalumu ya kuwahudumia wafanyakazi," alisema.

Alisema hali hiyo itatoa mfano bora kwa taasisi nyingine na chachu kwa wafanyakazi kwa kujituma zaidi na kwa ubora na hata wale wachache ambao walikuwa wakilegalega, wataongeza juhudi zaidi.



# Wakulima kahawa wapata faida zaidi

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WAKULIMA wa kahawa katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameanza kunufaika na programu maalumu ya kuongeza faida ya zao hilo.

Programu hiyo inalenga kuongeza tija kwenye uzalishaji, ubora wa mazao pamoja na kuwaunganisha wakulima hao na masoko.

Uboreshaji wa zao hilo unafanywa na Programu ya AGRI-CONNECT ambayo inalenga kuboresha mnyororo wa thamani wa zao hilo chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Akizungumza kwenye mkutano huo, kiongozi wa timu ya watekelezaji wa Programu hiyo, Colin Scott, alisema inalenga kuboresha maeneo sita ya mnyororo wa thamani wa zao la kahawa.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni pamoja na kusaidia kuboresha sera na mazingira ya biashara ya zao hilo, kuongeza tija kwenye uzalishaji na usindikaji uboreshaji wa miundombinu ya barabara za vijijini ili kuwaunganisha wakulima na masoko, maghala, viwanda na kurahisisha usafirishaji wapembejeo za kilimo.

Vilevile, Scott alisema programu hiyo inalenga kusaidia kuongezeka kwa uwekezaji hasa wa sekta binafsi kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo, kuongeza ajira kwa wanawake na vijana pamoja na kusaidia kuhamasisha lishe bora.

"Programu hii, mbali na kutekelezwa katika mikoa hii ya Nyanda za Juu Kusini, inatekelezwa Zanzibar na katika maeneo haya yote programu inatarajia kuwafikia wakulima wadogo 150,000," alisema Scott.

Alisema programu pia imejikita kuboresha mnyororo wa thamani wa chai na mazao ya bustani.

Vile vile, alisema programu hiyo inanatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau wa sekta binafsi.

Alisema mkutano huo pia ulilenga kujadiliana namna ya kuondoa mwingiliano wa shughuli miongoni mwa wadau wanaoshiriki kuwasaidia wakulima ili kuepuka kuwachanganya wakulima hasa taasisi hizo zinapofanya kazi zinazofanana.

Akielezea ufadhili Umoja wa Ulaya katika mnyororo wa thamani wa zao la kahawa mwakilishi wa Jumuiya hiyo, Andrea Massarelli, alisema Tanzania ina fursa nyingi kwenye sekta ya kilimo.

Alisema Tanzania ina ardhi ya kutosha inayoweza kusaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwamo kahawa na ndio sababu ya Jumuiya hiyo kufadhili.

"Jumuiya ya Umoja wa Ulaya imejikita katika kusaidia uongezaji wa tija na ufanisi wa sekta ya kilimo hasa kwenye zao la kahawa," alisema Massarelli.

Baadhi ya wadau wa mnyororo wa thamani wa kahawa walisema ubora wa kahawa inayozalishwa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini umeanza kuongezeka na hivyo kuwa na uhakika wa soko lenye faida.

Mmoja wa wadau hao, Sandra Ca'rdenas, mwakilishi wa Taasisi ya usambazaji wa teknolojia za kisasa za usindikaji wa kahawa inayojulikana kama Msumbi Afrika JM ESTRADA kutoka Colombia, alisema ili kuongeza ubora zaidi wakulima wanatakiwa kutumia mitambo ya kisasa ya kusindika kahawa.

Wadau wenginge waliowasilisha mada kwenye mkutano huo ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Taasisi ya Mitaji ya Kilimo Biashara (Bamboo Agribusiness Capital) ya nchini Kenya pamoja na mashirika ya Solidaridad na Vi-Agroforestry yanayotekeleza miradi chini ya programu ya AGRI-CONNECT.

Kahawa ni miongoni mwa mazao ya biashara ambayo yanaliingizia taifa fedha nyingi za kigeni, lakini katika miaka ya karibuni uzalishaji ulianza kushuka hasa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutokana na sababu mbalimbali.



Mwakilishi wa jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU), Andrea Massarelli, akizungumza kuhusu ufadhili wa jumuiya hiyo kwenye programu ya AGRI-CONNECT inayolenga kuboresha mnyororo wa thamani wa zao la kahawa kwenye mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakati wa mkutano wa wadau wa zao hilo mwishoni mwa wiki, jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Washtakiwa madai ya wizi wa mamilioni

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imewapandisha kizimbani watumishi sita wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na mfanyabiashara mmoja kwa tuhuma kadhaa ikiwamo la ubadhirifu wa zaidi ya Sh. mlioni 75 za serikali zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anatoa taarifa ya utendaji kazi wa Taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari mpaka Machi, mwaka huu.

Aliwataja watumishi waliofikishwa mahakamani ni aliyekuwa Mwekahazina wa Halmashauri ya Rungwe, Christopher Nyaki, Mkuu wa Idara ya Ununuzi wa Halmashauri hiyo, Victoro Mwakapala na aliyekuwa Ofisa Utumishi wa Wilaya hiyo, Rebeka Msambusi.

Wengine ni aliyekuwa Ofisa Elimu wa wilaya hiyo, Joseph Mabeyo, aliyekuwa Mtunza Fedha wa Halmashauri hiyo, Anyosisye Mwankenjela, aliyekuwa dereva, Godfrey Mwasambili pamoja na mfanyabiashara, Nelson Mushi.

Alisema kosa hilo la ubadhirifu wa fedha za umma ni kinyume cha sheria namba 11 ya TAKUKURU ya mwaka 2007.

"Kosa la pili linalowakabili watumishi hawa ni la matumizi mabaya ya madaraka kinyume cha kifungu cha Sheria ya TAKUKURU namba 11 ya mwaka 2007 na kosa la tatu ni la kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri," alisema Matechi.

Alisema kesi dhidi ya watu hao inaendelea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Rungwe, huku akiwatahadharisha watumishi wengine kuacha tabia za aina hiyo.

Katika hatua nyingine, Matechi alisema katika kipindi cha miezi mitatu, TAKUKURU ilifanya operesheni mbalimbali na kuokoa zaidi ya Sh. milioni 127.6 ambazo zilitakiwa kufanyiwa ubadhirifu ama kuchepushwa kwa njia ya rushwa.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 71.6 zilikuwa ni mali ya vyama vya Ushirika (AMCOS), Sh. milioni 16.1 za watu binafsi, Sh. milioni 33.3 fedha za Halmashauri na Sh. milioni 6.4 za kodi.

Alisema kati ya fedha zilizookolewa kwenye SACCOS, Sh. milioni 13.1 zilikuwa mali ya Ernest Mwakapesa, mwanachama wa SACCOS ya Kiwira wilayani Rungwe ambazo aliziweka kama amana kwenye chama hicho, lakini kiongozi wake, Emil Massawe, alijimilikisha fedha hizo.

Pia, alisema baada ya maofisa wa TAKUKURU kupata taarifa hizo waliamua kuingia kazini kwa ajili ya kufuatilia na ndipo wakaziokoa fedha hizo na kuwatahadharisha viongozi wa vyama hivyo kuacha tabia ya kufanya ubadhirifu wa fedha za vyama.

# Mbarali yapunguza uhaba wa madawati

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, imepunguza uhaba wa madawati katika shule zake za sekondari kwa zaidi ya asilimia 80 baada ya Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Francis Mtega, kuamua kutumia fedha zote za mfuko wa jimbo kutengeneza madawati na kuyasambaza shuleni.

Mbunge huyo aliamua fedha zote zaidi ya Sh. milioni 70.9 zitumike kuchonga madawati na madawati 875 yalipatikana.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati hayo serikalini, Mtega alisema kuwa aliamua kuelekeza fedha hizo kwenye sekta ya elimu akiamini kuwa ina kero nyingi ambazo zinahitaji ufumbuzi wa haraka.

"Natambua kuwa jimbo langu linazo kero nyingi, lakini nimeamua nianze na kero za kwenye sekta ya elimu ambazo athari zake zinawakumba wazazi na watoto pia, lakini najua kuwa elimu ndio msingi wa maendeleo hivyo tukimaliza kero kwenye sekta ya elimu tutakuwa tumeweka mazingira mazuri ya kujiletea maendeleo," alisema Mtega.

Akipokea madawati hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema mahitaji ya madawati katika wilaya yote ya Mbarali ni makubwa na uamuzi alioufanya mbunge wa kuelekeza fedha za Mfuko wa Jimbo kwenye utengenezaji wa madawati ni mzuri wenye nia ya dhati ya kusaidia sekta ya elimu.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya elimu ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanaoandikishwa darasa la kwanza na wanaofaulu mtihani wa taifa wa darasa la saba wanapata vyumba vya madarasa wanapoanza masomo.

Mfune alishauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kutoa maelekezo kwenye ngazi ya kata ya kuwataka watendaji kukusanya michango ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na miundombinu mingine wakati wa mavuno ili kila mwananchi aweze kuchangia bila shida.

"Kwa kawaida tumekuwa tukikimbizana kujenga vyumba vya madarasa kuanzia mwezi wa 12 na Januari baada ya matokeo ya mitihani ya taifa kutangazwa, lakini kipindi hiki pia huwa ni wakati wa kilimo, nashauri michango ya ujenzi na hata ujenzi wenyewe uwe unaanza mapema kuanzia mwezi Juni au Julai wakati ambao pia wakulima huwa wana uwezo mzuri wa kuchangia kwa sababu huwa wako kwenye mavuno," alisema Mfune.

Alisema wananchi wanapotakiwa kuchangia kuanzia mwezi Desemba au Januari huwa wako kwenye msimu wa kilimo na pengine baadhi yao huwa wameshauza mazao muda mrefu na kutokuwa na fedha, jambo ambalo huathiri hata kasi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu.



# Vituo vya afya visivyosajiliwa vyaonywa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imevipa wiki moja vituo vya afya binafsi 12, kukamilisha taratibu za kisheria za usajili kabla ya kuvifungia.

Angalizo hilo lilitolewa kwa vituo hivyo baada ya kushindwa kukamilisha taratibu za kisheria za usajili na kuonywa kwamba baada ya wiki moja watakaoshindwa kutekeleza maelekezo hayo watafungiwa.

Akizungumza na baadhi ya wamiliki wa vituo hivyo, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazurui, alisema serikali haipendi kuvifungia vituo vya afya, lakini sheria za nchi lazima zifuatwe.

Alisema hospitali na vituo vya afya binafsi ni mdau na inathamini mchango mkubwa wanaotoa katika kuimarisha huduma za afya na itaendelea kutoa kila msaada na kuhakikisha wanawahudumia wananchi kwa ubora.

Waziri Mazurui aliwataka wamiliki wa vituo hivyo, binafsi kuendeleza ushirikiano na serikali na watakapobaini kuna sheria kandamizi wasisite kutoa mapendekezo kwa wizara na kuahidi yatafanyiwa kazi.

Msaidizi Mrajisi wa Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi, Khamis Makame Haji, alisema wamiliki wa hospitali walitakiwa kukamilisha taratibu za usajili mpya kwa mwaka 2021 mpaka kufikia Januari 15, lakini kutokana na matatizo yaliyojitokeza waliongeza muda mpaka Machi na baadhi walishindwa kufanya usajili huo.

Alisema bodi hiyo ilifanya juhudi kubwa ya kuwafuatilia na kuwahimiza wamiliki hao ili kuendeleza shughuli zao, hata hivyo, wengine walipuuza.

Baadhi ya wamiliki waliotakiwa kukamilisha taratibu za usajili mpya 2021 wameahidi kuwa katika kipindi hicho cha wiki moja watahakikisha wanatekeleza agizo walilopewa na waziri.

Wakati huo huo, Waziri wa Mazurui amepokea msaada wa dawa kutoka kampuni ya Wide Spectrum Limited ya Dar es Salaam. Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Khamis Saleh Fakir, alimkabidhi Waziri Mazurui, msaada huo na kusema ni sadaka yao kwa wananchi katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani.

Alisema ni wadau wa afya na wiki iliyopita walikuwa Pemba na walitoa msaada wa dawa Hospitali ya Wete na Chake Chake na wataendelea kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar kusaidia hospitali na vituo vya afya.

Waziri Mazurui aliishukuru kampuni hiyo kwa msaada wa dawa na kumueleza kuwa wizara inathamini watu wenye moyo wa kusaidia wananchi wenzao.



Meneja Masoko wa Kampuni ya Wide Spectrum Ltd ya Dar es Salaam, Khamis Saleh Fakir, akimkabidhi Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, msaada wa dawa kwa ajili ya vituo vya afya vya Unguja (kushoto) ni Mfamasia Mkuu Zanzibar, Habib Ali Sharif. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# KMKM yasukwa upya kuondoa makundi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Azana Hassan Msingiri, ametangaza kuvunja makundi yote yaliyokuwamo ndani ya kikosi hicho na kuweka nidhamu ya kazi kwa wafanyakazi wake.

Alisema hayo wakati akizungumza na maofisa na wapiganaji wa kikosi hicho baada ya kujitambulisha rasmi makao makuu ya KMKM, Kibweni.

Alisema makundi ndani ya taasisi ya kiaskari ni ukosefu wa nidhamu kwa mujibu wa sheria za jeshi na hatakuwa tayari kumvumilia yeyote atakayebainika kuwa na kundi ndani ya kikosi hicho.

Aidha, alisema ni jambo la msingi kwa wafanyakazi kwa sasa kufanya kazi kwa uadilifu ikizingatiwa kuwa Rais wa Zanzibar na Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ, Dk. Hussein Mwinyi, anakitegemea kikosi hicho katika suala la kuzuia magendo na watu wote wanaohujumu uchumi wa bahari.

Msingiri, alitoa onyo kwa wale wote wanaojihusisha na ulaji wa rushwa wakiwa katika kazi hizo au wanaowaachia wahalifu baada ya kupigiwa simu na wakubwa zao.

"Kwa hili nawaambia wazi tena kweupe nikija kumgundua mtu huyu anachukua rushwa au anashirikiana na wahalifu kuudhofisha uchumi wa nchi hatakuwa salama," alionya.

Alisema Serikali ya Zanzibar inawahudumia maaskari hao pamoja na vyombo vyao kwa kuwalipa mishahara kwa ajili ya kazi hiyo ya kuzuia magendo ili kuhakikisha wananchi wanalipa kodi kupitia bandari zilizowekwa kisheria.

Aliwataka kufanya kazi kwa nidhamu, uwajibikaji na kujituma kwa kufuata sheria na miongozo ya kazi ili kuleta maendeleo ya nchi na taifa kwa ujumla.

Akizungumzia kuhusu uzalishaji, alisema Rais Mwinyi ana matumaini na kikosi hicho katika kuzalisha kupitia baharini na ndiko kwenye shamba la kikosi hicho. Aliahidi kuanza kuvua na kufuga samaki ili kuzalisha na kutangaza kununua boti tano aina ya faiba ili kuanza kazi rasmi shughuli hiyo. Mkuu wa Operesheni KMKM, Kamanda Hussein Ali Makame, alisema kikosi kina maeneo mengi ya kuzalisha mali kupitia fursa mbalimbali walizonazo. Alisema KMKM iliwahi kutengeneza boti ya faiba moja ambayo wanaitumia sasa iliyoundwa baada ya mafunzo waliyoyapata kutoka kwa mtaalam ambaye walimpa kazi ya kuwafundisha ufundi huo.

Kamanda Hussein, alisema wataendelea kumtumia mtaalam huyo tena ili awafundishe kutengeneza makoti ya uokozi (life jacket), jambo ambalo litaisaidia kikosi hicho na kufikia lengo la kuunga mkono kwa vitendo juhudi za Rais wa Zanzibar kuzitaka idara hizo kuzalisha.

# Wakulima viungo, matunda wataja changamoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa kilimo cha viungo, mboga na matunda kiswani Pemba, wamesema ukosefu wa elimu ya kuzalisha mazao bora ni changamoto inayowakwamisha kuyafikia masoko na kushindwa kufikia malengo waliyoyakusudia.

Hayo yamebainishwa na wakulima katika kikao cha kujadili changamoto zinazowakabili wafanyabiashara kisiwani humo.

Walisema kutokana na elimu duni wanazalisha mazao yasiyokidhi viwango kulingana na mahitaji ya soko.

Mbarouk Mohamed Hamad, mmoja wa washiriki wa mkutano huo, alisema wapo wakulima na wafanyabiashara wenye utayari wa kuzalisha kwa wingi, lakini elimu ya usizalishaji wa mazao bora ni kikwazo zaidi ambacho kinasababisha kukata tamaa ya kuendelea na uzalishaji.

"Wakulima tuna bidhaa nyingi, lakini tatizo lipo kwenye kuzifikisha bidhaa hizo sokoni zikiwa na ubora wake na kutokana na kukosa elimu ya uzalishaji bora wakulima wengi bado hawaoni kama kilimo ni sehemu ya kuongeza kipato," alisema.

Mkulima, Dadi Omar Dadi, alisema changamoto nyingine ni uwapo wa tozo kubwa pamoja na gharama katika upatikanaji wa alama ya ubora wa bidhaa.

"Tunafahamu huwezi kulifikia soko kubwa kama huna nembo ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) na wakulima na wafanyabiashara wengi tunashindwa kufika huko kutokana na kukosa uthibitisho huo."

Akitoa maoni, Saleh Said Suleiman, alisema usawa katika uhamasishaji wa taasisi zinazosimamia mazao ya kilimo kwa wakulima kuzalisha mazao yote ni mdogo kutokana na wataalamu kuegemea kwenye baadhi ya mazao machache.

Ofisa kilimo Wilaya ya Chake Chake, Juma Khamis Rajab, alisema licha ya kuwapo kwa uhaba wa wataalam wa kilimo, hao wachache waliopo wengi wao hawana taaluma katika mazao mengi hasa viungo na matunda.

Dk. Salim Seleman Ali, kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), alisema wadau wana jukumu la kuungana pamoja kutoa maoni ya changamoto zinazowakabili katika sekta ya kilimo na biashara ili kuhakikisha lengo la kubadilisha sekta ya kilimo kuwa yenye tija kwa wakulima linafikiwa.

"Ili lengo la mradi huu wa viungo, mboga na matunda uweze kufanikiwa ni wajibu wetu wadau wa kilimo na biashara kuyazungumza matatizo yanayotukabili ili mwisho wa siku tujue namna ya kuyatatua," alisema.

Mapema ofisa anayeshughulika na kuwaunganisha wadau katika mradi huo, Arafa Abdalla Juma, alisema lengo la ujio wa mradi huo ni kuongeza upatikanaji wa masoko ili kuwezesha kilimo chenye tija kwa wakulima.

Kikao hicho ni mwendelezo wa utekelezaji wa mradi wa kilimo hicho Zanzibar unaotekelezwa na Chama cha Wandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) upande wa Zanzibar, People's Development Forums (PDF), na Community Forests Pemba (CFP), kupitia uhisani wa Umoja wa Ulaya (EU).

# Madiwani wamfukuza kazi mhasibu kwa kutoonekana kazini miaka miwili

**Na Said Hamdani,** LINDI

ILE kaulimbiu ya kazi iendelee iliyoanzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeanza kung'ata baada ya Baraza la Madiwani Manispaa ya Lindi, kufuta ajira ya mtumishi wake idara ya fedha, Luka Tesha, kwa madai ya utovu wa nidhamu ikiwamo utoro kwa muda mrefu.

Madiwani hao walichukua uamuzi huo kwenye kikao cha Baraza lao, kilichofanyika mjini hapa.

Akitangaza uamuzi huo mbele ya waandishi wa habari, mwenyekiti wa kikao hicho ambaye pia ni Meya wa manispaa hiyo, Frank Magari, alisema hatua ya kumfuta kazi mtumishi huyo imetokana na kutoonekana eneo lake la kazi kwa zaidi ya miaka miwili bila ya taarifa kwa mwajiri wake.

Magari alisema mtumishi huyo aliyeajiriwa kuhudumu nafasi ya mhasibu katika idara ya fedha kwenye halmashauri hiyo miaka sita iliyopita, hajaonekana eneo lake la kazi kuanzia mwaka 2019.

Alisema kutokana na kitendo hicho, madiwani kupitia kikao cha Baraza, wamechukua uamuzi wa kumfukuza kazi Tesha, ili nafasi hiyo iweze kujazwa na mtu mwingine na kazi iendelee.

"Baada ya mkurugenzi kuwasilisha taarifa ya mtumishi wetu huyu, na tukaijadili kwenye kikao na madiwani wakaona busara kufuta ajira yake," alisema Magari.

Kikao hicho pia, kimemuagiza mkurugenzi kufanya mchakato kwa ajili ya kupata mtu mwingine wa kuziba nafasi yake.



Baadhi ya wataalam mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, mkoani Iringa wakifuatilia mkutano wa Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Hospitali Dar yapata mfumo wa Oksijeni

**Na Beatrice Moses**

HOSPITALI ya Chanika iliyopo Ilala, jijini Dar es Salaam imekabidhiwa Sh. milioni 3.8 kwa ajili ya ufungaji wa mfumo wa Oksijeni.

Uwezeshaji huo umefanywa na Benki ya NMB kupitia kwa wafanyakazi wake Idara ya Treasury, kiasi hicho cha fedha kimechangwa na wafanyakazi hao na kukabidhiwa Jumamosi na ufungwaji wa mfumo wa Oksijeni katika hopsitali hiyo, utaokoa maisha ya mama na watoto, ambao wamekuwa na uhitaji mkubwa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi hundi hiyo, Mwakilishi wa Idara ya Treasury NMB, Samira Saleh, aliishukuru Ofisi ya Mganga Mkuu kwa ushirikiano uliofanikisha makabidhiano hayo, wanaamini msaada huo unaenda kuokoa maisha ya mama na mtoto wanaohudumiwa hospitalini hapo.

"Katika kuunga mkono jitihada za serikali za kupunguza vifo vya mama na mtoto, kama alivyotuasa Rais Samia Suluhu Hassan kuchangia harakati za kuwavusha salama mama na mtoto, tumeamua kuchangia kiasi hiki ili kufunga mfumo wa Oksijeni hapa, ili kusaidia takribani kinamama 30 wanaojifungulia hapa kila siku.

"Tunaamini msaada huu unaenda kujenga mazingira salama ya kimatibabu kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU), Neonatal Care Unit (NCU) na Emergency Unit, hivyo kupunguza uhitaji wa rufaa kwenda hospitali za rufani Amana na ya Taifa Muhimbili," alisema Samira.

Awali, akizungumza Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Willy Sangu, alisema Hospitali ya Chanika imekuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wanaohudumiwa hapo, hasa kutokana na ongezeko la watu na makazi eneo la Chanika, mfumo wa Oksijeni unaofungwa kwa msaada huo, utawasaidia wengi katika wodi mbalimbali, hasa kwenye kipindi hiki cha uwapo wa changamoto za upumuaji.

Wakati huo huo, benki hiyo imetoa msaada wa meza 60 na viti 60 kwa shule za msingi Mtambani na Mgeule, zilizopo Tabata, Ilala jijini Dar es Salaam, vyenye thamani ya Sh. milioni 14, huku ikitoa mabati 170 yenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa ajili ya shule shikizi Mnauka iliyoko Wilani Newala mkoani Mtwara.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema meza na viti hivyo ni sehemu ya mpango wao wa Uwajibikaji kwa Jamii, inayoendeshwa kwa miaka kadhaa sasa kupitia asilimia moja faida ya NMB kila mwaka, inayotumika kusaidia sekta za elimu, afya na majanga.

"Tunatoa meza 30 na viti 30 kwa kila shule, tukiamini msaada huu sasa unaenda kuboresha mazingira ya kufundishia kwa kuwaongezea ari ya utekelezaji wa majukumu yao waalimu wa Mtambani na Mgeule kwa ustawi wa elimu ya watoto wanaosoma hapa," alisema Richard.

Mkuu wa wilaya, Ndwata Ludigija alikiri kuwa sera ya elimu bure imeongeza idadi ya wanafunzi mashuleni, hivyo kusababisha changamoto nazo kuwa nyingi na kwamba Serikali inajivunia na kuhitaji uungwaji mkono kutoka kwa wadau wa sekta hiyo.

# Taasisi za ukopeshaji zaomba riba iongezwe

**Na Richard Makore,** MWANZA

TAASISI za fedha nchini zinazotoa mikopo midogo (Microfinance), zimeiangukia serikali na kuiomba kuongeza riba wanayotoza wateja wao ya asilimia 3.5 iliyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa madai kwamba inawaumiza.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, jijini hapa, Mwenyekiti wa taasisi hizo, Nyihita Nyihita, alisema BoT imeweka masharti kwa taasisi hizo kutoza riba isiyozidi asilimia 3.5 katika mikopo wanayotoa kwa wateja wao hatua ambayo haiwezi kuwapa faida.

Alisema gharama za kuendesha biashara hiyo ni kubwa ikiwamo kodi, ushuru wa leseni na mishahara ya wafanyakazi, na kuiomba serikali kufikiria kuondoa sharti hilo.

Alisema taasisi hizo ambazo zinafikia 600 kwa nchi nzima zinatoa mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi, na BoT ikiendelea kuweka sharti hilo watashindwa kujiendesha.

Alimuomba Rais Samia Suluhu Hassan, kufikiria suala hilo, huku akitoa mfano kwamba taasisi yenye mtaji wa Sh. milioni 20 ikikopesha zote kwa riba ya asilimia 3.5 itapata faida ya Sh. 700,000, kiasi ambacho alisema ni kidogo.

Alisema faida hiyo ikigawanywa kwenye kodi na ushuru mwingine haiwezi kutosha na taasisi hizo zipo hatarini kufunga biashara zao.

Hata hivyo, Nyihita hakusema wanataka riba hiyo iongezwe hadi kufikia kiasi gani, lakini aliomba serikali kuwaita na kujadiliana.

Aliongeza kuwa sheria hiyo imepitishwa mwaka 2018 ambayo imeanza kutekelezwa na BoT, lakini akaomba serikali kukutana na taasisi hizo kwa kuwa haikuwashirikisha katika suala hilo.

Hivi karibuni, serikali imekuwa ikipiga kelele kuhusu baadhi ya taasisi za fedha ambazo zinatoa 'mikopo umiza' huku zikiwafilisi baadhi ya wastaafu na wananchi waliokopa kwao.

**Faida hiyo ikigawanywa kwenye kodi na ushuru mwingine haiwezi kutosha na taasisi hizo zipo hatarini kufunga biashara zao.**

# HABARI KIMATAIFA

## Mazungumzo mpango wa nyuklia Iran yaahirishwa

**Vienna,** AUSTRIA

AWAMU ya tatu ya mazungumzo na Iran juu mpango wake wa nyuklia, yaliyokuwa yanafanyika mjini Vienna, Austria yameahirishwa.

Wajumbe wa Ulaya walisema wasiwasi wao juu ya kuzorota kwa mazungumzo hayo.

Lengo la mazungumzo hayo ni kuirudisha Marekani katika makubaliano yaliyofikiwa mwaka 2015 kati ya Iran na mataifa makubwa sita.

Wajumbe wa Ujerumani, Ufaransa na Uingereza ambayo ni mataifa yaliyo sehemu ya mkataba huo wa nyuklia walisema licha ya kwamba kila upande umeonyesha utayari wa kuurejesha mkataba huo, uliotiwa saini mwaka 2015, hatua zilizopigwa hadi sasa hazijafika mbali.

Tangu mwanzoni mwa Aprili, mwaka huu, wanadiplomasia hao pamoja na wengine kutoka China na Urusi, walikutana mjini Vienna kwa mazungumzo ya kujaribu kuishawishi Marekani kurejea kwenye mkataba wa nyuklia na Iran baada ya aliyekuwa rais wa nchi hiyo Donald Trump, kuiondoa nchi yake kutoka kwenye mkataba huo mwaka 2018.

Iran ambayo pia inashinikizwa kuheshimu masharti ya mkataba huo, ilisema bado kuna tofauti kubwa kuhusu masuala muhimu, itaendelea kushiriki kwenye duru nyingine ya mazungumzo wiki ijayo. Kwa upande wake Urusi ilionyesha kuwa na tahadhari wakati huo huo, ikieleza juu ya kuongezeka kwa matumaini ikisema matokeo madhubuti huenda yakapatikana katika muda wa wiki tatu.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Abbas Araghchi anayeongoza ujumbe wa Iran alisema mazungumzo hayo yanatia moyo, ingawa hatua zaidi zinahitajika.

Araghchi alitaka vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa dhidi ya Iran viondolewe.

Iran iliwekewa vikwazo katika sekta za nishati, fedha, viwanda vya magari, mabenki, bima na masuala ya bandari.

**DW**

## Wanawake milioni 60 walipoteza kazi duniani

**Geneva,** USWISI

ZAIDI ya wanawake milioni 64, walipoteza kazi zao kote duniani, mwaka jana kutokana na mlipuko wa janga la corona.

Kulingana na ripoti mpya ya shirika lisilo la kiserikali la Oxfam International, ilibainishwa kuwa janga hilo liliathiri zaidi wanawake.

Mwaka jana, wanawake hao walipoteza kazi zao kutokana na janga hilo na kupoteza mapato ya dola bilioni 800, sawa na mapato ya ndani ya nchi 98.

Mkurugenzi Mtendaji wa Oxfam International, Gabriela Bucher alisema upotezaji wa mapato hayo haujumuishi upotevu wa mamilioni ya wanawake ambao wanapata ajira isiyo rasmi kama huduma za nyumbani, masoko, ushonaji.

Ripoti hiyo pia ilibainisha kuwa inakadiriwa wanawake milioni 47 zaidi wataangukia kwenye umaskini uliokithiri mwaka huu.

**TRT**

# Kenyatta alegeza marufuku ya kutotoka nje Nairobi

**Nairobi,** KENYA

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ameondoa katazo la watu kuingia au kutoka katika kaunti tano, lililowekwa kwa ajili ya kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona.

Maeneo yaliyowekewa katazo hilo yalikuwa ni Nairobi, Nakuru, Machakos, Kimabu na Kajiado.

Rais aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya sikukuu ya wafanyakazi duniani juzi.

Wakati alipotoa agizo la pili kwa umma Machi mwaka huu, jinsi ya kukabiliana na janga la corona, Nairobi ilikuwa na jumla ya maambukizi 56,815.

Rais Kenyatta alisema Maambukizi yalipungua Aprili, mwaka huu, hadi kufikia 15,000, ikionyesha maambukizi kupungua mjini Nairobi kwa asilimia 74.

Alisema takwimu za wataalamu wa afya zinaonyesha hali kama hiyo katika eneo ambalo lililowekwa amri ya watu kutotoka nje Machi 26, mwaka huu. "Baada ya mwezi mmoja wa marufuku ya kutoka nje, kesi za maambukizi ya Covid-19 zilipungua mpaka asilimia 72," alisema Kenyatta.

Pia rais alisema maeneo mengine ya nchi, maambukizi ya yamepungua kwa asilimia 89 mjini Mombasa na Busia yakipungua kwa asilimia 90, kuanzia Machi na April, mwaka huu.

**DW**



Wakazi wa mji wa Kabul nchini Afghanstan, wakishuhudia malori kadhaa ya mafuta yaliyoungua na kuua watu saba, Kaskazini ya mji huo, huku watu 14 wakipelekwa hosptalini baada ya kujeruhiwa, jana. PICHA: AP

# Kiongozi utekaji nyara wanafunzi 300 auawa

**Lagos,** NIGERIA

KIONGOZI mashuhuri wa genge lililojihusisha na vitendo vya utekaji nyara wa wanafunzi zaidi ya 300 Desemba, mwaka huu, ameuawa na mahasimu wake.

Auwalu Daudawa, aliripotiwa kuvamiwa wakati akijaribu kuiba kundi la ng'ombe kutoka kwa kundi lenye silaha katika jimbo la Kaskazini Magharibi la Zamfara.

Daudawa anadaiwa kutekeleza vitendo vya utekaji nyara wa mwezi Desemba katika jimbo la Katsina.

Alipewa msamaha kama sehemu ya makubaliano ya amani, , Februari mwaka huu, ingawa inasemekana alirudi kwenye genge lake mapema wiki hii.

Chini ya makubaliano ya Februari, Daudawa alisamehewa katika jimbo la Zamfara, baada ya kusema alitubu na kukabidhi silaha zake kwa serikali.

Wanachama wa genge lake la uhalifu waliahidiwa makazi na Gavana wa jimbo, Bello Matawalle, pamoja na msaada wa kusaidia kuboresha maisha yao.

Ijumaa, wiki iliyopita, Daudawa na washirika wengine wanne wa genge lake, walipigwa risasi baada ya majibizano makali katika msitu uliopo karibu na mpaka na Katsina, ofisa wa eneo hilo aliliambia shirika la habari la AFP.

"Aliwaongoza watu wake kwenye harakati za kulipiza kisasi kifo cha wafuasi wake wawili na genge hasimu wakati wa uvamizi ulioshindwa katika moja ya kambi zake mwezi uliopita," afisa huyo aliongeza.

Utekaji nyara wa mamia ya watoto wa shule katika jimbo la Katsina mwezi Desemba, ambao ulidaiwa kuongozwa na genge la Daudawa, ulikuwa moja wapo ya uvamizi uliodaiwa kulenga kupata malipo ya kikombozi.

Wanafunzi hao waliungana tena na familia zao wiki moja baada ya kutekwa nyara.

Serikali baadae ilisisitiza hakuna fidia iliyolipwa wakati huo, wavulana waliachiliwa baada ya mazungumzo na watekaji nyara.

Kikundi cha wanamgambo wa Kiislam Boko Haram, kilisema wakati huo kilikuwa kilitekeleza vitendo vya utekaji na kwamba kiliajiri magenge ya eneo hilo kutekeleza shambulio hilo.

Boko Haram, awali ililenga shule kwa sababu ya upinzani uliopo dhidi ya elimu ya 'Kimagharibi' ambayo wanaamini inavunja miiko ya Uislamu.

Jina la kundi hilo lina maana kuwa ''Elimu ya Magharibi ni haram''

**BBC**

# UNDP laonya ongezeko la umasikini Myanmar

**Washington,** MAREKANI

SHIRIKA la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa-(UNDP), limeonya kuwa karibu nusu ya idadi ya watu wa Myanmar, wataingia kwenye umasikini mapema mwakani.

Hali hiyo inatokana na athari za kiuchumi, kijamii na virusi vya corona na mapinduzi ya kijeshi ya Februari mwaka huu.

Ripoti iliyotolewa na UNDP, ilisema mapato yanashuka kwenye sehemu kubwa ya sekta za viwanda, ikiwamo biashara ya rejareja, kilimo na uvuvi kutokana na kuenea kwa maambukizi.

UNDP ilisema karibu watu milioni 12 huenda wakaingia kwenye umasikini na kusababisha watu milioni 25, karibu nusu ya idadi ya watu nchini hapa, kuishi chini ya mstari wa umasikini wa taifa, kufikia mapema mwaka 2022.

Kiwango cha umasikini cha Myanmar kilikuwa chini kwa asilimia 24.8 mwaka 2017.

**NHK**



# KLOPP: KEITA BADO YUPO KWENYE MIPANGO YANGU

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp ameweka wazi kwamba, Naby Keita anabaki kwenye mipango yake ya muda mrefu hapo Liverpool, licha ya kiungo huyo kukabiliwa na wakati mgumu msimu huu klabuni hapo.

Majeraha yamemfanya Keita kuwa kwenye wakati mgumu tangu alipojiunga na timu hiyo akitokea RB Leipzig.

Na kumekuwa na uvumi kwamba, nyota huyo huenda akaondoka mwishoni mwa msimu huu kutokana na kutokuwa na namba ya kudumu kikosini hapo.

Lakini Klopp amebainisha kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea bado yupo kwenye mipango yake.

"Bado yupo kwenye mipango yangu ya muda mrefu, ataendelea kuwa hapa na kupata nafasi ya kucheza kila itakapobidi," alisema Klopp kabla ya mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Manchester United.

"Majeraha kwa kiasi kikubwa yamemfanya kuwa nje ya uwanja, lakini kwa uhakika kabisa yupo kwenye mipango ya muda mrefu ya timu hii."

# ZIDANE AMPA NAFASI VARANE KWA CHELSEA

**MADRID, Hispania**

RAPHAEL Varane ana majeraha madogo, kwa mujibu wa Zinedine Zidane, ambaye ana matumaini mlinzi huyo wa kati atakuwa fiti kwa ajili ya mchezo dhidi ya Chelsea wiki hii.

Varane alitolewa nje kipindi cha pili kwenye mchezo dhidi ya Osasuna Jumamosi, wakati Madrid wakiibuka na ushindi wa 2-0 kwa mabao ya 'jioni' kutoka kwa Eder Militao na Casemiro.

Ushindi huo umewafanya Madrid kupunguza pengo hadi pointi mbili dhidi ya vinara wa LaLiga Atletico Madrid, ambao waliwafunga Elche kwenye mchezo wa mapema.

Huku Los Blancos hao wakiwakabili Sevilla waliopo nafasi ya nne kwenye msimamo wiki ijayo, na Barca wakicheza na Atletico, mbio za ubingwa wa ligi hiyo zinaonekana kuwa ngumu.

Hata hivyo, kutolewa kwa Varane kwenye mchezo huo kulikuwa na lengo la kumuweka salama kuelea mchezo dhidi ya Chelsea na Sevilla.

Madrid watacheza na Chelsea pale dimba la Stamford Bridge kwenye nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikiwa ni baada ya mchezo wa kwanza kutoka sare ya kufungana bao 1-1. Na Zidane ana matumaini Varane atakuwa fiti kwa ajili ya mchezo huo.

"Sijui, tunatakiwa kusubiri," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "Ameniambia mimi kwamba ni kitu kidogo. Natumaini si tatizo kubwa."

# RONALDO ATAFUTA TIMU YA KUHAMIA

**TURIN, Italia**

NYOTA wa kikosi cha Juventus, Cristiano Ronaldo, dili lake la kurejea Real Madrid linaonekana kushindikana na sasa ameanza kutafuta timu nyingine.



Hivi karibuni taarifa zilieleza kwamba, Ronaldo yupo kwenye hesabu za kurudi Madrid ila timu yake hiyo ya zamani iliamua kumpotezea kwa kueleza kuwa haina mpango naye kwa sasa.

Mkataba wake ndani ya Juventus umesalia muda wa mwaka mmoja na mengi waliyotarajia mabosi wake kupata kutoka kwake yameshindikana jambo ambalo linaonyesha kwamba hataongezewa mkataba.

Katika Ligi ya Mabingwa Ulaya imeshindwa kufanya vizuri baada ya kutolewa na hawana nafasi ya kutwaa ubingwa wa Serie A jambo ambalo linaongeza ugumu kwa staa huyo kubaki katika timu hiyo.

Wakala wa mchezaji huyo, Jorge Mendes, alishakutana na bodi ya Manchester United na inaonekana itakuwa ngumu kurudi, pia timu nyingine inayotajwa ni PSG nayo inawania saini ya nyota huyo.

Kwa mujibu wa Sky Sport Italia, uwezekano wa Ronaldo kuendelea kucheza hapo Juventus kwa msimu mwingine ni ngumu, kwani sasa akili yake ni kutaka kuondoka na kutafuta changamoto kwingineko.

HABARI MICHEZO

# Cavani kusaini mkataba mpya

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Kimataifa wa Uruguay, Edinson Cavani, ametajwa kuwa yupo mbioni kukubali ofa aliyopewa na vigogo wa Manchester United ya kuongeza mkataba wa mwaka mwingine mmoja wa kuendelea kuitumikia miamba hiyo ya soka la England.

Cavani mwenye umri wa miaka 34, alijiunga na Man United, Oktoba mwaka jana akitokea Paris St-Germain kwa kusaini mkataba wa mwaka mmoja wenye kipengele cha kuongeza miezi mingine 12.


Inasemekana mshambuliaji huyo alikuwa na mpango wa kuondoka, lakini kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer alivunja ukimya Alhamisi kwa kusema anahitaji kumwona akisalia kwenye kikosi chake.

Kwa mujibu wa BBC Sport, imefichuka kwamba, Solskjaer amechangia kwa kiasi kikubwa kwa Cavani kubadili maamuzi yake na yupo tayari kwa sasa kuendelea kusalia Old Trafford.

Miongoni mwa mambo ambayo yanatajwa kumtibua Cavani na kutamani kuondoka England ni baada ya kipindi fulani kufungiwa kwa kile kinachosemekana kwamba alijihusisha na ubaguzi kupitia mitandao ya kijamii.

Licha ya kutoa ufafanuzi kwamba hakuwa na maana ovu, chama cha soka England kilimweka hatiani na kumbidi raia huyo wa Uruguay kukosa michezo kadhaa huku akilipa pia faini kutokana na kosa hilo la kibaguzi.

Kulikuwa na tetesi kwamba Boca Juniors ya Argentina ilikuwa na mpango wa kumrejesha nyumbani, America ya Kusini mshambuliaji huyo ambaye alitupia mabao mawili kwenye mchezo uliopita wa nusu fainali ya Europa Ligi na kutoa asisti tatu wakati Man United ikiibuka na ushindi wa 6-2 dhidi ya AS Roma.





# VAN DIJK AANZA MAZOEZI LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk, ameanza kuwapa furaha mashabiki wa timu yake baada ya kuweka video mtandaoni ikimuonyesha akifanya mazoezi ya kukimbia ikiwa ni mwendelezo wa kurejea uwanjani.

Beki huyo raia wa Uholanzi amekuwa nje ya uwanja tangu Oktoba mwaka jana baada ya kuumia goti wakati alipogongana na kipa wa Everton, Jordan Pickford.

Baada ya kuumia ilielezwa kuwa atakosa msimu wote huu wa 2020/21 uliosalia, lakini video hiyo imeanza kuonyesha mwanga mzuri wa kurejea kwake. Kwa hatua ilivyo sasa kuna uwezekano wa kurejea katika moja ya mechi tano za mwisho kabla ya msimu kumalizika.

Van Dijk alikuwa akifanya mazoezi hayo katika viwanja vya mazoezi vya Liverpool, ambapo baada ya hapo video hiyo ilipata maoni mengi hasa kutoka kwa mashabiki wa timu yake.

Kukosekana kwa Van Dijk kumekuwa na pengo kubwa kwa kuwa timu yake imeyumba katika safu ya ulinzi kiasi cha kumvuruga kichwa Kocha Jurgen Klopp hasa kwa kuwa pia alipata majeruhi wengine kadhaa katika nafasi ya ulinzi.

# *Klabu zilizotaka kuanzisha ligi mpya kuadhibiwa*

**NYON,** Uswisi

RAIS wa Shirikisho la Soka Ulaya (Uefa), Aleksander Ceferin, amethibitisha klabu zote 12 zilizotaka kushiriki mashindano mapya ya 'European Super League' zitaadhibiwa.

"Pamoja na mpango wao wa kutokufanikiwa, sisi kama shirikisho hatutakaa kimya tutawafundisha somo jipya kwa kuwaadhibu," alisema Ceferin.


"Hatutaki kujua nani alikuwa kinara wa mpango huu, wala nani alikuwa wa kwanza kujiondoa katika jambo hili, hivyo tutatoa adhabu kwa wote."

Alipodadisiwa juu ya aina ya adhabu wanazotarajia kuzitoa, alisema, "hili litajadiliwa kwa kina japo kwa upande wa Uingereza huenda ikazidi kwa kuwa ilihusisha vurugu za mashabiki kupinga jambo hili japo nadhani haitaenda mbali na adhabu ya faini."

Kuliibuka taharuki kubwa juu ya kuanza kwa mashindano mapya ya Ulaya ambayo yalitafsiriwa yanakuja kukinzana na mashindano yaliyo chini ya UEFA kwa kuwa klabu zote zilizotangaza kushiriki huwa zinacheza michuano hiyo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER HANA MPANGO UNITED KUMUUZA POGBA

●●● Hapana, bila shaka hapana, mara zote nimesema nikiwa na Paul nafurahia kuinoa...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesisitiza anataka kumbakiza Paul Pogba wakati huu kukiwa na uvumi kuhusu majaliwa yake klabuni hapo.

Pogba mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na kumekuwa na maswali kuhusu majaliwa ya nyota huyo wa Ufaransa, tangu wakala wake, Mino Raiola alipodai Desemba mwaka jana kuwa muda wa mteja wake kukaa hapo United umefikia mwisho.

Akiwa anahusishwa na mpango wa kurudi Juventus na kwenda Real Madrid, Pogba amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia pale United, ambao wapo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu na wana nafasi ya kutinga fainali ya Kombe la Ligi ya Europa baada ya kushinda 6-2 dhidi ya Roma, kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali.

**"Hapana, bilashaka hapana," alisema Solskjaer wakati alipoulizwa kama angependa kumuuza Pogba mwishino mwa msimu huu.**

"Mara zote nimesema kwamba, nikiwa na Paul nafurahia kuinoa timu hii, nafurahia kuzungumza naye na pia nafurahia kumpa changamoto yeye kwa sababu ni mshindi.

"Anataka kuwa bora na ndio maana anasikiliza. Unaweza kuona anafurahia yeye mwenyewe.

"Anatabasamu kwenye uso wake. Ni muhimu kila mmoja anamjali mwenzake kwa heshima.

"Lakni kuna baadhi ya wachezaji unawajua tangu wakiwa vijana wadogo, ndivyo ilivyo kwa Paul."

Pogba amefunga mabao sita katika mashindano yote kwa United msimu huu, yakiwamo matatu kwenye Ligi Kuu.

## ZISIKUPITE

### AGUERO AGEUKA LULU

EVERTONA imeungana na Chelsea, Leeds United, Tottenham, Barcelona na Inter Milan katika mbio za kutaka kumsajili straika wa Argentina, Sergio Aguero, ambaye atakuwa huru mwishoni mwa msimu huu pale Manchester City. ***(Star on Sunday)***

### SALAH BADO LIVERPOOL

STRAIKA wa Misri, Mohamed Salah, amesema Liverpool haijazungunza naye kuhusu kuongeza mkataba mpya klabuni hapo, huku ule wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ukiwa unamalizika kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2023. ***(Sky Sports)***

### DE BEEK HAUZWI

MANCHESTER United itakataa ofa yoyote kwa ajili ya kiungo wake, Donny van de Beek mweye umri wa miaka 24. ***(Sun on Sunday)***

### BISSOUMA ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inaamini kwamba wanaweza kumsajili kiungo wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 24 kwa pauni milioni 30. ***(Star on Sunday)***

### ABRAHAM AWANIWA MILAN

AC Milan inamfuatilia kwa karibu straika wa Chelsea na England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, ambaye pia anatakiwa na West Ham. ***(Standard)***

### MARTINEZ KURUDI EPL

KOCHA wa timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez, atakuwa tayari kurudi kwenye Ligi Kuu England - na anahusishwa na Tottenham Hotspur. ***(Sun on Sunday)***

### PARKER ATAJWA SPURS

KOCHA wa Fulham, Scott Parker, pia anatajwa kuwa kwenye orodha ya kuchukua mikoba ya Jose Mourinho aliyefukuzwa, pale Tottenham, ambako aliwahi kuicheza kwa miaka miwili. ***(Football Insider)***

### FLICK ATAKA UKOCHA

KOCHA anayeondoka Bayern Munich, Hansi Flick anataka kuwa kocha mkuu wa Ujerumani wakati Joachim Low atakapoondoka baada ya michuano ya Euro 2020, kuliko kwenda Tottenham Hotspur. ***(Sport1)***

### RAMOS ANA MIAKA MIWILI

KIUNGO wa Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 35, bado ana matumaini ya kuongeza miaka miwili pale Real Madrid, ambapo wamempa ofa ya mwaka mmoja. ***(Marca)***

### DONNARUMMA KUTUA JUVE

WAKALA wa golikipa wa Italia, Gianluigi Donnarumma, ambaye mkataba wake na AC Milan unamalizika mwishoni mwa msimu huu, Mino Raiola, amefanya mazungumza na Juventus kuhusu nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 ili kujiunga nao. ***(Calciomercato)***

## HABARI MICHEZO

# UTALII WA MICHEZO SASA NDANI YA HIFADHI YA TAIFA YA MIKUMI

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HIFADHI ya Taifa ya Mikumi iliyopo Wilaya ya Kilosa mkaoni Morogoro, imeanzisha viwanja vya michezo na kuboresha vilivyopo ili kuwezesha kuwa na utalii wa michezo itakayoongeza hamasa ya utalii kwa watalii wa ndani na nje ya nchi kushiriki michezo mbalimbali ukiwamo mpira wa miguu.

**Kupitia kuanza kwa ujenzi huo, Hifadhi ya Mikumi, imezialika klabu kubwa hapa nchini ikiwemo Simba, Yanga na Azam kutumia viwanja hivyo pale vitakapokamilika kwa ajili kufanya mazoezi ya maandalizi ya michezo yao ya ndani na nje kwa kuwa vitakuwa na ubora unaokubalika ndani na kimataifa.**

Kamishna Mwandamizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi Tanzania (TANAPA) Kanda ya Mashariki, Asteria Ndaga, aliyasema hayo mbele ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii iliyotembelea hifadhi hiyo.

Kamati hiyo iliyokuwa chini ya Mwenyekiti wake, Aloyce Kwezi, ikiwa na mwenyeji wao Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ilitembelea hifadhi hiyo ili kuona utoaji wa huduma mbalimbali kwa watalii na uboreshaji miundombinu wezeshi.

Kamishana huyo Mwandamizi wa Uhifadhi, Ndaga alisema, kuanzishwa kwa utalii wa michezo ni utekelezaji wa maelekezo ya Waziri wa wizara hiyo, Dk. Damas Ndumbaro, ambaye mapema miezi ya hivi karibuni aliuagiza uongozi wa hifadhi hiyo kuanzisha utalii wa michezo.

Alisema, tayari kazi hiyo imeanza kutekelezwa kwa uboreshaji wa uwanja wa mpira wa miguu uliopo na kuanzisha viwanja vipya viwili vya michezo ya mpira wa kikabu (basket ball) na mpira wa nyavu (volley ball) ikiwa ni pamoja na kubadilisha ukumbi wao mmoja kuwa eneo la mazoezi ya viungo vya mwili (gym) kwa watalii wanaotembelea hifadhi hiyo.

Kamishna huyo mwandamizi wa uhifadhi, alisema utalii wa michezo ni kipaumbele cha kipekee katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, ambayo mtalii anaweza kuona wanyama wa aina mbalimbali kwa wakati mmoja na pia ni rahisi kufikika.

"Ndani ya uhifadhi kutakuwa na viwanja vya kisasa vya michezo mbalimbali kama mpira wa miguu, mpira wa pete, na michezo mingine kama mpira wa kikapu ambavyo itachezwa huku wanyama wakiwa ndani ya Hifadhi Taifa ya Mikumi, tunasisitiza michezo kufanyika hapa, tunataka kubadilisha kabisa utalii wa hifadhi hii, ili mtalii akifika anapata fursa ya kufanya mazoezi wakati wanyama wakiwa karibu," alisema Ndaga .

Alisema tayari walikuwa na uwanja wa mpira wa miguu, hivyo kutokana na kupaumbele hicho, kwa sasa wameazisha viwanja vya mchezo mingine.

**ITAKUWA HIVI...**




Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini, wakati huu timu hiyo ikitarajiwa kushuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi kuvaana na watani wao wa jadi, Simba, kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

# *Chama abeba tuzo mchezaji bora Aprili*

**Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Mzambia Clatous Chama, ameibuka mshindi wa tuzo ya mchezaji bora wa Mashabiki wa mwezi Aprili.

Katika tuzo hizo zinazodhaminiwa na Emirate Aluminium ambazo zilianza hivi karibuni kwa lengo la kuwaongezea morali wachezaji wa timu hiyo kufanya vizuri, Chama amewabwaga Aishi Manula na Shomari Kapombe.

Mchezaji wa kwanza kutwaa tuzo hiyo alikuwa ni winga raia wa Msumbiji, Luis Miquissone na wa pili akiwa ni beki kisiki wa kati, Joash Onyango.

Chama ambaye amekuwa miongoni mwa wafungaji wa Simba walioiwezesha kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara na kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, alitangazwa jana kuibuka mshindi wa tuzo hiyo kupitia ukurasa rasmi wa klabu ya hiyo.

Hadi sasa katika Ligi Kuu Bara, Chama amecheka na nyavu mara saba huku akitoa pasi za mwisho 13, wakati huu Simba ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu na pointi zake 61 zilizotokana na mechi 25.

Pia Simba ndiyo timu inayoongoza kwa ufungaji mabao 58 kati ya hayo saba yakiwa ya Chama, huku timu hiyo ikiruhusu nyavu zake kutikishwa mara 10 tu.

Simba ambayo juzi iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Benjamin Mkaka, Jumamosi itashuka tena uwanjani hapo kuikaribisha Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu.

## Kagera yageukia kubaki Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Kagera Sugar, Manyika Peter, amesema wanaenda kujipanga kwa ajili ya kupambana kupata matokeo mazuri ili kujinusuru kushuka daraja msimu ujao.

Kagera Sugar juzi usiku iliondolewa kwenye hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho nchini (FA Cup) kwa kukubali kichapo cha mabao 2-1, kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Manyika alisema mechi ilikuwa nzuri kipindi cha kwanza, lakini Simba iliwazidi kipindi cha pili na kuwaondoa katika mashindano hayo na sasa wanaenda kujipanga kwa ajili ya mechi zilizobakia za Ligi Kuu.

Alisema wameona makosa yao na wako katika nafasi mbaya kwenye msimamo wa ligi kwa sasa, hivyo wanafanyia kazi upungufu wao ili kupata matokeo chanya katika michezo iliyobaki mbele yao.

"Tunakubali Simba walituzidi kipindi cha pili, sasa tunahitaji kufanya vizuri katika ligi, hatuhitaji kupoteza mechi zetu zilizobaki ili kuendelea kuwapo katika ligi kwa msimu unaokuja," alisema Manyika.

Kagera iko nafasi ya 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 27 sawa na JKT Tanzania inayoshika nafasi ya 17 na Mwadui FC akiburuza mkia na alama zake 19.

## Umitashumta, Umisseta kivumbi Singida Mei 29

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MICHEZO ya Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na ile ya Umoja wa Michezo wa Shule za Sekondari nchini (UMISSETA) kwa Mkoa wa Singida, inatarajiwa kuanza kutimua vumbi kuanzia Mei 29-31, mwaka huu katika viwanja vya Shule ya Sekondari Mwenge.


Afisa Maendeleo ya Michezo wa Mkoa wa Singida, Henry Kapera, ndiye aliyetoa taarifa hiyo juzi mbele ya wanahabari kuelekea maandalizi ya mashindano hayo.

Kapera alisema wachezaji watakaochaguliwa kuunda timu ya mkoa wataingia kambini kuanzia Juni Mosi hadi 3, kabla ya kuondoka kwenda kwenye mashindano hayo yanayotarajiwa kuanza Juni 6-19, mwaka huu.

# Michezo

Jumatatu Mei 3, 2021

Nipashe

SOLSKJAER HANA MPANGO UNITED KUMUUZA POGBA

HABARI UK 22

POLE MKUU...



Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akimuinua winga Bernard Morrisson, baada ya kuifungia timu yake bao la kusawazisha dhidi ya Kagera Sugar na kujigonga katika mlingoti wa goli kwenye mechi ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na Simba kushinda 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Gomes hesabu zote kwa Yanga kwanza

## ●●●Amtaja Morrison huku akifunguka ya Kaizer Chiefs, Onyango naye asema...

**Na Saada Akida**

HUKU akiwapongeza nyota wake kwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho nchini (FA Cup), Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema kwa sasa hawataki kupoteza mechi yoyote, hivyo anaziandaa silaha zake kwa ajili ya mchezo ujao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga utakaopigwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba juzi usiku ilitinga robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Kagera Sugar, kwa ushindi wa mabao 2-1, shukrani kwa wafungaji, Bernard Morrison na Meddie Kagere.

Akizungumzia na gazeti hili jijini jana, Gomes amewasifu wachezaji wake kutokana na uwezo walioonyesha kwa kutoka nyuma na kusawazisha kabla ya kupata bao la ushindi, lililowaweka katika nafasi nzuri ya kuelekea kutetea ubingwa wao huo.

Alisema walimiliki sehemu kubwa ya mchezo kipindi cha kwanza na kucheza vizuri, lakini hawakuwa na bahati ya kufunga jambo lililomlazimu kufanya mabadiliko ya kiufundi kipindi cha pili ambayo yalizaa matunda.

"Niliamua kubadili mbinu kwa kuwatumia washambuliaji wawili, Meddie Kagere na John Bocco ili kuongeza mashambulizi, upande wa viungo pia nilimuingiza Bernard Morrison, aliweza kutimiza majukumu kwa wakati na kuwafanya Kagera Sugar washindwe kuhimili kasi yetu," alisema Gomes.

Alisema baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali, sasa wanaelekeza nguvu katika mechi ijayo dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga, na ni muhimu kushinda kwa kuwa unaamua mustakabali wa ubingwa msimu huu.

"Kuelekea mchezo dhidi ya Yanga sisi morali yetu ipo juu, tumetoka kucheza mechi sita na kushinda zote na mechi hii itaonyesha nani atakuwa bingwa kwa hiyo ni vizuri kushinda mechi hiyo dhidi ya Yanga," alisema Gomes.

Alisema hawezi kuweka wazi mipango yake na kuhusu Morrison ambaye amekuwa mchezaji muhimu kwa kuisaidia timu hiyo kumuanzisha katika mechi ijayo dhidi ya Yanga.

Alisema hana mashaka na uwezo wa Morrison, lakini pia hawezi kuwashutumu washambuliaji wake hasa Kagere kukosa nafasi nyingi, hivyo ana imani atafanikiwa kutumia nafasi na kufunga mabao kwenye mechi zijazo na kuendelea kuwa juu ya kwa ufungaji.

Naye beki wa Simba,Joash Onyango, alisema wanachokifikiria kwa sasa ni mechi yao dhidi ya Yanga na si Kaizer Chiefs ambayo watacheza nayo kati ya Mei 14-15, mwaka huu.

"Tunashukuru tumeingia robo fainali na sasa hatuwezi kuwazungumzia Kaizer Chiefs wakati tuna mechi nyingine hivi karibuni dhidi ya Yanga, sasa tumemaliza FA tunaenda kujiandaa dhidi ya Yanga," alisema Onyango.

Alisema ana imani itakuwa mechi ya ushindani kwa sababu timu zote zinahitaji matokeo ila kwao watahitaji pointi tatu muhimu kwa ajili ya kuendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba ambao ni wenyeji wa mchezo huo, ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 61, nne mbele ya Yanga iliyopo mebe kwa michezo miwili.

# NTIBAZONKIZA AWATOA YANGA WASIWASI J'MOSI

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mechi ya watani wa jadi dhidi ya Simba, mshambuliaji tegemeo wa Yanga, Said Ntibazonkiza, amewatoa wasiwasi mashabiki wa timu hiyo baada ya kueleza kwamba anaamini watapata matokeo.

Katika michezo miwili iliyopita wakati wakipokea kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Azam FC kwenye Ligi Kuu na kisha kwenda kupata ushindi kama huo dhidi ya Tanzania Prisons hatua ya 16-bora ya Kombe la FA, Ntibazonkiza amekuwa chaguo la kwanza chini ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi ambaye ameiongoza timu hiyo kwenye mechi hizo.

Kiungo huyo mshambuliaji raia wa Burundi amekuwa na uwezo mkubwa wa kucheza na mpira na kupiga mipira ya adhabu akisaidiaina na Carlos Carlinhos.

"Sifuatilii mechi za wapinzani wangu hao, mimi sijui ila kikubwa tunachoangalia ni mechi zetu na kuona tunapata matokeo, hakuna jambo lingine.

"Kuhusu kucheza sina wasiwasi pale ambapo ninapata nafasi hivyo ni suala la kusubiri na kuona itakuajе," alisema.

Kama Ntibazonkiza atacheza itakuwa mechi yake ya kwanza dhidi ya watani hao wa jadi, Simba kuichezea Yanga.

Simba yenye alama 61 na mechi mbili mkononi, ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiizidi Yanga kwa pointi tatu.




GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002